# Nipashe

Jumatatu Septemba 19, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581073

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US









**Gari** la jeshi ladaiwa kuua, utata waibuka mochwari

UKURASA 5



## GREALISH AMSHUKURU GUARDIOLA

UKURASA 22



# 'Panya Road' walivyouawa

• **Risasi** zatumika kuwakabili mitaani...

*Endelea ukurasa 2*



Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Murilo, akionyesha moja ya silaha zilizokamatwa katika msako wa wahalifu wa mitaani, maarufu Panya Road, alipotoa taarifa kwa waandishi wa habari jana.
**PICHA: JUMANNE JUMA**

## YALIYOMO


UKURASA WA 2

**SAMIA MMOJA WA WAGENI MAALUM MAZISHI YA MALKIA**

RAIS Samia Suluhu Hassan yuko jijini London, Uingereza kwa ajili ya kushiriki...

UKURASA WA 3

**ASHIKILIWA KWA TUHUMA MAUAJI YA ALIYELALA NAYE**

MKAZI wa Kijiji cha Kiroka, wilayani Morogoro, Salipina Thomas (21), anashikiliwa na polisi kwa tuhuma za mauaji...

UKURASA WA 4

RIPOTI MAALUM -2

**MTOTO ALIYEFUNGIWA NDANI ALIVYONAJISIWA NA KUAMBUKIZWA VVU**

KATIKA sehemu ya kwanza ya ripoti hii jana, kulikuwa na simulizi ya kijana aliyenajisiwa na baba yake mdogo na hata...


## CHADEMA na wadau wakumbusha Katiba Mpya

UKURASA 7



# Ndalichako ashtukia upigaji wa mamilioni ya UVIKO-19

UKURASA 3


**MICHEZO** **MAYELE AAHIDI MAKUNDI CAF** UK.24 **KABWELA** UK.18

## LHRC yashinda kesi kutetea wanaopata ujauzito shuleni

**Na Maulid Mmbaga**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimeshinda kesi iliyofungua mwaka 2019 dhidi ya serikali kwa Kamati ya Afrika ya Wataalamu ya Haki na Ustawi wa Mtoto, kuwatetea wasichana wanaopata ujauzito wakiwa shuleni na kunyimwa nafasi ya kuendelea na masomo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi na Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Wakili Anna Henga, katika shauri hilo waliwasilisha mambo matano yanayovunja haki za wasichana ikiwamo vipimo vya mimba vya lazima kwa wasichana shuleni.

Mengine ni kufukuzwa kwa wasichana wanaopata ujauzito na walio kwenye ndoa shuleni, kuwazuia wanaopata ujauzito kurudi shule hata pale wanapojifungua, kuwafunga watoto wanaopata ujauzito na kuendelea kuwahukumu watoto ambao wamenyanyaswa na kufanyiwa ukatili na kutokuwa na elimu na taarifa sahihi ya afya ya uzazi shuleni. Alisema hayo yanasababisha uvunjifu wa haki za wasichana kama ilivyoainishwa kwenye Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto.

"Haki zilizobainishwa kwenye mkataba huo ni ya elimu, usawa na kutobaguliwa, haki ya kulindwa dhidi ya masuala ya kijamii yenye madhara, maslahi mapana ya mtoto, afya pamoja na upatikanaji wa afya ya uzazi, faragha na haki ya kuwa huru dhidi ya ukatili, unyanyasaji na mateso," alisema Anna.

Kamati hiyo ilidai mwongozo ulioandaliwa na serikali haukukidhi vigezo vya ulinzi wa haki za wasichana kama ilivyoainishwa kwenye mkataba wa Afrika wa haki na ustawi wa mtoto ambao Tanzania iliridhia.

**UPUNGUFU WA MWONGOZO**

Alisema kamati hiyo ilibainisha upungufu wa mwongozo kuwa haujazungumzia masuala muhimu yaliyowasilishwa, ikiwamo upimaji mimba wa lazima na kufukuzwa wasichana shuleni wanapopata ujauzito.

Mwongozo kutoweka wazi kuhusu wasichana waliofukuzwa shuleni na umeelezea kuhusu wanafunzi wanaoacha masomo kwa sababu mbalimbali, ikizingatiwa kanuni za elimu zinazoruhusu ufukuzwaji wa wasichana kwa kigezo cha maadili, ambazo bado zinatumika.

Kuwa na ukomo wa muda kwa kuwa unaruhusu wanafunzi waliocha shule miaka miwili kabla ya mwongozo na haki za wasichana waliowakilishwa katika kesi hiyo kuendelea kuvunjwa. Pia, haujasema lolote kuhusu kufutwa kwa Sheria ya Elimu na sheria nyingine kandamizi ikiwamo pia utungwaji wa sheria au sera ya kuwaruhusu watoto kurudi shule.

**MAPENDEKEZO YA KAMATI**

Alisema, kamati hiyo iliamuru serikali kukomesha upimaji wa ujauzito wa lazima shuleni, kupitia Sheria ya Elimu ya 2002 pamoja na kanuni zake na kuondoa mimba pamoja na ndoa za utotoni kama vigezo vya kuwafukuza watoto shule.

Pia serikali kuchukua hatua stahiki kuzuia watoto wa kike kufukuzwa shule wanapoingia kwenye ndoa au kupata ujauzito na badala yake kuwekwa sheria mahususi na sera kuwalinda dhidi ya ndoa na mimba za utotoni. Kamati ilipendekeza kufutwa kwa sera zinazozuia watoto kurudi shule, ikiwamo sababu za mimba au ndoa.

Aidha, serikali iwaruhusu watoto walionyimwa nafasi ya elimu kwa sababu hizo kurudi shule haraka iwezekanavyo na kuwafidia kwa muda wote waliopoteza.

Iliomba serikali itoe mwongozo kwa wakuu wa shule na wasimamizi wa elimu wasichana wanaoacha shule kwasababu ya mimba au ndoa waruhusiwe kurudi shule na ifanyie uchunguzi kesi za watoto wa kike waliowekwa gerezani kwa sababu ya mimba na kuhakikisha wanaachiwa na kuacha kuwaweka ndani wasichana wanaopata ujauzito. Kadhalika, kamati hiyo ilipendekeza kutolewa huduma rafiki za elimu ya afya ya uzazi kwa wasichana balehe, kutoa elimu kwa walimu, wahudumu wa afya, polisi na watendaji wengine kuhusu wasichana wanaopata ujauzito au walioingia kwenye ndoa.

Pia ilishauri kuchukua hatua za muhimu kuondoa ndoa za utotoni, kuchukuliwa hatua stahiki kuhusu ukatili wa kijinsia, ubaguzi, umaskini, mila na desturi zilizopitwa na wakati na kuweka mifumo ya utoaji taarifa kwa waathirika wa ukatili wa kingono ikiwamo ndoa za utotoni na kutoa msaada wa kisaikolojia kwa wahusika.

Kamati hiyo vile vile, ilipendekeza kufanya uchunguzi na kuwachukulia hatua wanaoshtakiwa kwa ndoa za utotoni na ukatili wa kingono na watu wote wanaohusika na upimaji wa mimba wa lazima na wanaowabagua wasichana kuhusu hali yao ya mimba na ndoa.

Pendekezo la mwisho ni kutoa huduma maalum kwa wasichana wanaopata ujauzito na walioingia kwenye ndoa kuendelea na elimu katika shule watakazopenda, pia imeitaka Tanzania kuchukua hatua hizo ndani ya siku 180 tangu kutoka kwa hukumu hiyo na kuhakikisha inawasilisha taarifa ya utekelezaji wa hukumu katika kamati.

# Polisi yaua 'panya road' sita

**Na Maulid Mmbaga**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Saalam, limeua vijana sita wanaosadikiwa kuwa ni 'panya road' waliokuwa wanakwenda eneo la Kinzudi, kufanya uhalifu wa kuvamia mtaa na kupora.

Vijana hao ni kati ya tisa waliokamatwa katika mapambano na polisi, kati yao sita walijeruhiwa na kufariki dunia wakati wakipelekwa hospitalini kwa matibabu.

Akifafanua kuhusu tukio hilo jana, Kamanda wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, alisema saa 4:15 usiku juzi, walipata taarifa kutoka kwa wananchi kwamba kuna kikundi cha wahalifu waliokuwa kwenye Noah yenye namba za usajili T 260 BEP wanaotoka Mabibo wakiwa na silaha wakielekea Goba Kinzudi kwa lengo la kufanya uvamizi.

Alisema baada ya kupokea taarifa hizo, ufuatiliaji wa haraka ulianza na askari polisi walipofika eneo la Makongo walikutana na gari hilo na walipolizuia ili kuwakamata wahalifu hao walishuka na kuanza kuwatishia polisi kwa mapanga ili wasikamatwe.

"Katika mazingira hayo askari walijihami kwa kufyatua risasi kadhaa hewani, lakini wahalifu hao waliendelea kukaidi na kutaka kuwajeruhi polisi, ndipo walishambuliwa na kujeruhiwa na baadaye walipelekwa haraka hospitalini, lakini kwa bahati mbaya walipoteza maisha," alisema na kuongeza:

"Wahalifu watatu katika purukushani hizo walifanikiwa kukimbia na Jeshi la Polisi linawasaka na litawakamata haraka iwezekanavyo, uchunguzi wa awali umebaini kuwa watu wawili kati ya wahalifu hao Salum Mkwama (30), mkazi wa Mbagala na Khalfan mkazi wa Buguruni, waliwahi kushtakiwa kwa kesi ya unyang'anyi wa kutumia silaha mwaka 2021 na baadaye kuachiwa kwa sababu mbalimbali za kisheria," alisema Muliro.

Kadhalika, Kamanda Murilo alisema watuhumiwa hao walikutwa na mapanga sita, visu viwili na vifaa vingine vya kuvunjia nyumba, akibainisha kwamba upelelezi wa awali pia umebaini kuwa watuhumiwa hao wanadaiwa kushiriki tukio la mauaji lililotokea Kawe Septemba 14, mwaka huu.

Alisisitiza kuwa jeshi hilo litaendelea kutekeleza maelekezo yaliyotolewa na Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP) Camillius Wambura ya kwamba mifumo ya usalama na kisheria inazingatiwa ili kuhakikisha hali ya usalama inarejeshwa haraka iwezekanavyo jijini Dar es Salaam. Pia alisema Jeshi la Polisi linaendelea kusimamia operesheni kali dhidi ya vikundi vinavyojihusisha na uhalifu katika maeneo mbalimbali ya jiji la Dar es Salaam, huku akiwaomba wananchi kuendelea kutoa taarifa za haraka ili wahalifu hao wadhibitiwe haraka kabla ya kutenda uhalifu.

"Polisi pia wanahimiza wananchi kuimarisha vikundi vya ulinzi shirikishi na jeshi linatoa tahadhari kwa wahalifu kuacha mara moja matukio ya kihalifu na watakaokaidi watakamatwa kwa kadri mazingira ya kisheria yatakavyoruhusu na kushughulikiwa kwa mujibu wa kisheria," alisisitiza Muliro.

Kutokana na tishio la panya road katika maeneo mbalimbali nchini, Alhamisi iliyopita, wabunge walitaka serikali kuchukua hatua madhubuti kuyadhibiti makundi ya vijana yanayoendesha vitendo hivyo na kutishia hali ya amani na usalama wa raia na mali zao.

Wabunge hao waliomba Bunge liahirishe ratiba yake na badala yake lijadili jambo la dharura kuhusu makundi hayo ambayo walisema baadhi ya wabunge pia wamevamiwa na kuathiriwa mali zao.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Akson, aliiagiza serikali kushughulikia jambo hilo kwa haraka.

Alisema serikali ina uwezo wa kuchukua hatua kwa kuwa taifa lilishapata hizo changamoto na serikali ilifanyia kazi na hayo mambo yakaisha kabisa na anaamini hata hilo ina uwezo wa kulimaliza.



Baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Waliul ASR Boys Seminary Kibaha Mpakani mkoani Pwani, wakipanda mboga katika bustani juzi baada ya kupata mafunzo ya kilimo cha mboga na matunda kwa Mkurugenzi wa Kampuni ya Matungullu's Mindset Changing And Entrepreurship, Amani Michael. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Samia mmoja wa wageni maalum mazishi ya Malkia

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS Samia Suluhu Hassan yuko jijini London, Uingereza kwa ajili ya kushiriki mazishi ya Malkia Elizabeth II.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Zuhura Yunus, jana viongozi mbalimbali walioalikwa akiwamo Rais Samia, walitoa heshima za mwisho kwenye eneo la holi la Westminster na kutia saini kitabu cha maombolezo.

Kwa mujibu wa Yunus, baada ya hapo, Rais Samia alitarajiwa kuhudhuria hafla fupi iliyoandaliwa na aliyetamkwa kuwa Mfalme Charles III ambaye amemrithi mama yake, Malkia Elizabeth II.

Hafla hiyo ambayo pia iliandaliwa na Malkia Mfariji, Camilla Parker Bowles, ilifanyika katika Kasri ya Buckingham katika jiji hilo la London. Taarifa hiyo ilibainisha kuwa leo Rais Samia atahudhuria mazishi ya kitaifa ya Malkia huyo yatakayofanyika kwenye Kanisa la Westminster Abbey na mwili wa Malkia Elizabeth II utalazwa kwenye Kasri la Windsor.

Malkia Elizabeth II anatajwa kama kiongozi aliyetoa huduma kwa muda mrefu zaidi nchini humo na alipitisha Uingereza katika nyakati ngumu na nyepesi katika kipindi chote cha utawala wake wa miaka 70.

Malkia alifariki dunia Septemba 8 mwaka huu akiwa na umri wa miaka 96 na Kasri la Buckingham ndiyo ilitangaza kwamba alifariki dunia akiwa katika Kasri ya Balmoral huko Scotland ambako alikuwa anapumzika katika majira ya joto.

Kabla ya kifo chake siku hiyo, kuanzia mchana familia ya kifalme ilianza kukusanyika kwenye kasri hilo baada ya taarifa kutolewa kwamba malkia alikuwa chini ya uangalizi wa matabibu wake kwa kuwa hali yake kiafya ilikuwa imedhoofika kwa kiwango kikubwa.

## HABARI KITAIFA

# Ndalichako ashtukia upigaji wa mamilioni

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako, ameibua ubadhirifu wa mamilioni ya shilingi yaliyotolewa kutokana na mkopo wa UVIKO-19 kwa ajili ya ukarabati wa Chuo cha Ufundi Stadi na Marekebisho kwa Watu Wenye Ulemavu Sabasaba.

Kufuatia ubadhirifu huo, ameiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kufanya uchunguzi katika chuo hicho kuangalia matumizi ya zaidi ya Sh. milioni 800 zilizotolewa kwa ajili ya ukarabati wa chuo.

Ubadhirifu alioubaini ni katika ununuzi wa vifaa vya ujenzi ambavyo vimenunuliwa kwa bei kubwa kuliko uhalisia, kuweka makadirio makubwa ya mahitaji ya vifaa vya ujenzi (BOQ) na kutopelekwa kwa baadhi ya vifaa katika chuo hicho wakati inaonyesha fedha zilishatolewa kwa ajili ya kununua.

Prof. Ndalichako aliibua ubadhirifu huo baada ya kufanya ziara ya siku moja katika wilaya za Manyoni, Ikungi na Singida juzi kukagua miradi inayotekelezwa na serikali kupitia wizara yake.

"Hapa kuna vimelea vya ubadhirifu kwa sababu mtu ana malengo gani kuweka mifuko 2,900 ya saruji halafu hauleti chuoni? Kwa hiyo, suala hili lazima lipelekwe TAKUKURU lichunguzwe, haiwezekani vitu havijafika lakini fedha yote imeshatumika," aliagiza.

Prof. Ndalichako alitoa mchanganuo wa vitu ambavyo vina utata kuwa ni matofali yaliyokuwa yanatakiwa katika ujenzi ni 7,000 lakini kwenye BOQ waliandika 14,700 na fedha ilishatolewa.

Aliongeza kuwa bei ya saruji iliandikwa kuwa ni Sh.18,000 bila Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na pia kwenye BOQ iliandikwa itatumika mifuko 2,912 wakati inayotakiwa kwa ajili ya kazi hiyo ni mifuko 900 tu kwa mujibu wa mkandarasi, lakini fedha ilishatolewa ya mifuko 2,912.

Kuhusu nondo, waziri huyo alisema iliandikwa zinahitaji 1,198 lakini uhalisia zinazohitajika ni nondo 50 tu, lakini pesa iliyotolewa ya nondo 1,198 na bei iliyowekwa kwa nondo moja ni Sh. 8,000 badala ya Sh. 5,000.

Alisema vioo vimenunuliwa kwa Sh.120,000 lakini kwenye BOQ imeandikwa vimenunuliwa kwa Sh. 220,000, jambo ambalo linaondoa maana halisi ya kutumia 'force account' (mfumo wa kutumia nguvukazi ya ndani).

"Kwa ujumla kazi hii haifai hata kidogo, vitu havipo katika uhalisia kabisa na BOQ iliyotumika kwenda kuombea fedha haiwiani na jinsi vifaa vilivyonunuliwa, hapa itabidi watu wa ununuzi watusaidie. Je, huu mfumo wa 'force account' umezingatiwa?" alihoji.

Prof. Ndalichako alisema shida kubwa katika mradi huu vitu vya kununua viliwekwa vingi kuliko uhalisia, mfano vikiwekwa vifaa vya kuanzishia kazi kwamba yatanunuliwa mashoka 22, majembe 22, makoleo 22, nyundo 22 na matoroli 22 na fedha ilishatoka lakini hakuna hata kitu kimoja kilichotoka.

Pia alisema marumaru zinazohitajika kwa ajili ya kazi hiyo ni maboksi 900 lakini fedha iliyotoka ni ya maboksi 1,105 na pia bei ya mabati imeandikwa kuwa yamenunuliwa kwa Sh. 99,120 lakini chuo kilinunua kwa Sh. 60,000 tu.

Aliongeza kuwa katika mchanganuo wa gharama za ukarabati wa chuo hicho, ilikuwa ziletwe Sh. milioni 812 lakini zimeongezwa na kufikia Sh. milioni 862 na kwamba jambo hili halikubaliki.

"Rais amekuwa akisisitiza watendaji kuwa makini katika utendaji wetu kila senti ya serikali tuilinde, lakini hapa unauliza hakuna maelezo, kila unayemuuliza anasema 'sijui', sasa kwanini anayejua asingekuja atoe maelezo maana hii ziara yangu haikuwa ya kushtukiza," alisema.

Mkuu wa Chuo cha Ufundi Stadi na Marekebisho kwa Watu Wenye Ulemavu Sabasaba, Fatma Malenga, kila alipoulizwa na waziri kuhusu utata wa ununuzi wa vifaa hivyo, alisema mambo mengi yalikuwa yanafanywa na watu wa wizarani hivyo hajui lolote.

# Ashikiliwa kwa tuhuma mauaji ya aliyelala naye

**Na Idda Mushi**, MOROGORO

MKAZI wa Kijiji cha Kiroka, wilayani Morogoro, Salipina Thomas (21), anashikiliwa na polisi kwa tuhuma za mauaji baada ya mwanaume aliyekuwa amelala nyumbani kwake, Rashid Maharagande, kuuawa na mtu aliyetoweka.

Tukio hilo limethibitishwa na Kamanda wa Polisi wa Mkoa, SACP Fortunatus Musilimu, wakati akizungumza na waandishi wa habari. Alisema lilitokea Septemba 17, mwaka huu, majira ya saa nane usiku kitongoji cha Temekero, Kijiji cha Kiroka, Tarafa ya Mkuyuni.

"Kijana Richard Stephen Chanzila (23), mkazi wa kitongoji cha Maembe, Kijiji cha Kiroka, ndiye anatuhumiwa kufanya mauaji hayo kwa kumkata kwa kitu chenye ncha kali shingoni kijana Maharagande, mkazi wa Sultan Area, Manispaa ya Morogoro aliyekuwa pia akijishughulisha na kazi ya bodaboda," alisema Musilimu.

Alisema chanzo cha mauaji hayo ni wivu wa kimapenzi baada ya Maharagane kukutwa amelala ndani ya nyumba ya Salipina, aliyekuwa na mahusiano naye ya kimapenzi.

Kamanda alisema baada ya mtuhumiwa kuwakuta wamelala, aliamua kumkatakata kwa kitu chenye ncha kali Maharagande sehemu ya shingoni.

Alisema wakati mwanamke huyo akikimbia kutafuta msaada, mtuhumiwa Chanzila aliubeba mwili wa marehemu na kuondoka nao kwenda kuutupa porini umbali wa karibu mita 100 kutoka eneo yalikofanyika mauaji.

Kamanda alisema mtuhumiwa anayedaiwa kuwa ni mzazi mwenzie Salipina, alitoroka kijijini hapo kwenda kusikojulikana baada ya mauaji hayo na polisi wanaendelea na msako ili kumtia mbaroni na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria. Aliwasihi wananchi kuacha kushiriki mauaji ya aina mbalimbali ikiwamo yanayosababishwa na wivu wa kimapenzi, ushirikina au migogoro mingine kwa kuwataka wafuate njia sahihi za kupata suluhisho la migogoro yao.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Temekelo 'A' Banzi Bonzo, akizungumzia mauaji hayo, alisema: "Yule binti ni jirani yangu na anaishi kwenye mtaa wangu, binti alikuwa na mwanaume aliyekuwa amezaa naye, lakini waliishi kwa malumbano mara nyingi na mara ya mwisho tuliwapeleka kituo cha Polisi Mkuyuni baada ya mwanaume kumtishia mwanamke kisu."

"Sijui kesi iliishaje, hadi usiku saa nane mzazi mwenzie naye alikuwa bado anamuwinda huyu binti bila kujua akamfuatilia na kuona ameingia na mwanaume mwingine kutoka Sultan Area mjini, ilikuwa hata hawajafanya kitu, akawavamia na kuwalazimisha kuvua nguo na kuanza kuwapiga mapanga, mwanamke akakimbia," alisema Banzi Bonzo.

Alidai majira ya saa moja asubuhi alifika jirani anayekaa karibu na nyumbani kwake na kutoa taarifa ya kuona damu nyingi nje ya nyumba yake. Alisema, walipoifuatilia ilifika hadi mlangoni kwa binti, na walipomtafuta hakuwapo nyumbani kwake na kuamua kwenda kwa mama yake mzazi anayeishi jirani na kumkuta binti aliyedai kuwa alikuwa anataka kwenda kwake kumjuza yaliyojitokeza usiku.

"Nilimuuliza mbona hakuja kwangu, kama aliweza kwenda kwa mama yake? Kwa kuwa ni lazima kwanza apite kwangu, lakini alianza kwa mama yake ndiyo atake kuja kwangu?" Akasema alichanganyikiwa baada ya kuona mwenzake waliyelala naye anapigwa mapanga."


KILIMANJARO CO-OPERATIVE BANK LIMITED
Together, Transforming Lives

**TAARIFA KWA UMMA NA WATEJA WETU**

UONGOZI WA BENKI YA USHIRIKA KILIMANJARO (KCBL) UNAWATANGAZIA WATEJA WOTE JUU YA MABADILIKO YA TAREHE YA KUFANYA MABORESHO YA MFUMO WAKE WA KIBENKI. MABORESHO YATAFANYIKA SIKU YA JUMAMOSI YA TAREHE 24-09-2022 BADALA YA TEREHE 17/09/2022 KAMA TULIVYO TANGAZA HAPO AWALI. MABORESHO YATAFANYIKA KUANZIA SAA 2:00 USIKU TAREHE 24/09/2022 HADI SAA 10:00 ALFAJIRI YA TAREHE 25-09-2022.

MABORESHO HAYA YATAATHIRI MFUMO MKUU WA BENKI NA UPATIKANAJI WA HUDUMA KWA WATEJA KUANZIA SAA 2:00 USIKU 24-09-2022 HADI SAA 10:00 ALFAJIRI YA 25-09-2022. MIFUMO NA HUDUMA ZITAKAZO ATHIRIKA NI PAMOJA NA MASHINE ZA KUTOLEA FEDHA (ATM) NA HUDUMA KUPITIA KWA MAWAKALA.

HUDUMA ZOTE ZITAREJEA ALFAJIRI YA TAREHE 25 SEPT, KUANZIA SAA 11.00. UONGOZI UNAOMBA RADHI KWA USUMBUFU WOWOTE ULIOJITOKEZA. PIA TUNAWASHAURI WATEJA KUPATA HUDUMA KABLA AU BAADA YA MUDA WA MABORESHO.

**IMETOLEWA NA MENEJA MKUU WA BENKI YA USHIRIKA KILIMANJARO (KCBL)**
**16 SEPTEMBA 2022**

117051402



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
19.09.2022

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kutaarifu umma kuwa siku ya Jumatano tarehe **21- 09 – 2022** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** . itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port kuelekea Rufiji**, gari hizo zenye namba za usajili: **T 203 DYJ / T 887 DJB T 135 CCP / T 837 DJB**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita 22** |
| **Upana** | - | **mita 4.5** |
| **Kimo** | - | **mita 5.0** |

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, Pwani hadi Rufiji** kupitia Kibiti, gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

217051502



**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

Chanzi Edmund Makongoro Kaondo mkazi wa Halmashauri ya mji wa Bariadi Mkoani Simiyu anatangaza kupotelewa na kadi ya gari iliyopotea nyumbani kwake, gari hilo ni aina ya Toyota **RAV4** yenye namba za usajili **T. 268 DBY.** Hivyo yeyote atakayeiona kadi hiyo apeleke taarifa katika kituo chochote cha polisi kilichopo mkoani Simiyu. Taarifa ya kupotea kwa kadi hiyo, imetolewa septemba **16/2022** katika kituo cha polisi cha Maswa kwa namba: **SIM/MAS/RB/368781/2022.**



The land Disputes Courts ( The District Land and Housing Tribunal) Regulations GN.No. 174/2003

(GN. NO. 943 Contd) *FOMU MIRADTHI -2*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya KIGOMA**
**Kituo cha MWANDIGA Mkoa wa KIGOMA**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 35 /2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU JOSEPH LAZARO KASEBA WA KAGONGO**
**KATIKA SHURI LA MAOMBI YA KUMTEUA YALIYOLETWA**
**NA JULIETH KASEBA MATETE**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5 (2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa nauhusiano wowote/ maslahi yoyoteya mirathi ya marehemu tanjwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 20 Mwezi 10 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

- Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani na unaweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika

**Imetolewa leo Tarehe 15 Mwezi 9 Mwaka 2022**

MAHAKAMA YA MWANZO WILAYA YA KIGOMA
HAKIMU MKAZI MFAWIDHI



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURI-(SUMMONS)**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO- USHIROMBO**

**WILAYA YA BUKOMBE**

**SHAURI LA MADAI 43/2022**

**KWA PASTORY MADUHU**
**WA USHIROMBO-BUKOMBE**
**K.K M/KITI WA KITONGOJI**

**Kwa kuwa imelazimika uhudhurie ili FIKA KUJIBU PINGAMIZI LA KUKAMATIWA MALI**

Unaamriwa na JAMHURI uhudhurie mbele ya mahakama hii siku ya IJUMAA tarehe 30/09/2022 saa Asubuhi na ukifika na usitoke bila ruksa ya mahakama.

Unaonywa kwamba ikiwa utashindwa kufika/kupokea wito huu au kupuuza bila udhuru wa maana. Hati itatolewa kukulazimisha kuhudhuria na utashtakiwa kwa kosa hilo.

Hati hii imetolewa kwa AMRI yangu na MHURI wa mahakama hii leo tarehe 16/09/2022

# Mtoto aliyefungiwa ndani alivyonajisiwa, apata VVU

**KATIKA sehemu ya kwanza ya ripoti hii jana, kulikuwa na simulizi ya kijana aliyenajisiwa na baba yake mdogo na hata kupata maambukizo ya VVU, pia athari wanazozipata watoto wanaofungiwa ndani kwa lengo la kukwepa ukatili dhidi yao ulioko nje ya makazi yao. Endelea kufuatilia mwendelezo wa ripoti hii.**

**Na Romana Mallya**

**KUTOKA KWA MWALIMU**

Mwalimu wa Shule ya Msingi Tumaini Kawe A, Wilaya ya Kinondoni mkoani Dar es Salaam, Alfonce Mwanyika, anashuhudia ukatili kwa wanafunzi wake, baadhi ndiyo hayo yenye ukakasi.

Mwanyika anasema wakati akiwa Shule ya Msingi Kumbukumbu alikokuwa anafanya kazi kabla ya kuhamishiwa Tumaini, alishuhudia hayo na ushawishi mkubwa unaotumika kwa watoto, ni zawadi ndogo ndogo kutoka kwa wakubwa, lakini akionyesha namna utamaduni umefika pabaya, hata mtoto kwa mtoto hutendeana.

"Kesi za namna hii zinapotufikia, huwa tunamwita mzazi na kumshirikisha, lakini wakitoka na kwenda kwenye Dawati la Jinsia kinachofanyika ni kwamba unakuta kesi inaisha bila ya kuwa na mwafaka.

Anaeleza mbinu binafsi inayomsaidia kuwagundua watoto ambao ama wamefanyiwa ukatili wa kijinsia au binafsi wanapokwenda kinyume cha tabia, ni namna wanapokuwa nao darasani.

"Wakati unafundisha unaona mtoto amekaa upande. Ukimuuliza mtoto mbona hukai vizuri, anakwambia 'ninaumwa', anasingizia labda anaumwa mguu, lakini, ukikaa naye kama rafiki, ukimnunulia vitu vidogo vidogo kama andazi anaanza kukusimulia 'mwalimu kuna mchezo mbaya nimefanyiwa'.

"Mwingine anakwambia 'kuna babu mmoja huwa ananishika na kunifanyia mchezo mbaya', mwingine anasema 'mwalimu fulani (anataja jina) ananifanyia hivi'.

"Ukifuatilia uwaite wenzake wakija, wanakataa lakini mwisho wa siku wanakiri kwamba wao walikuwa wanafanya hivyo, kama sehemu ya michezo yao," anasimulia mwalimu huyo huku akibeba hisia za wazi, amejawa na ukakasi wa kinachotokea dhidi ya wanafunzi wake.

Anaeleza pale wanapochukua hatua ya kufuatilia pande zote mbili za wazazi, siri inafichuka kwamba ni matukio ya anayeharibu na kuharibiwa wote ni majirani na ndiyo mwanzo wa mjadala kuondoa polisi na ukarejeshwa mtaani walikotoka.

Hata hivyo, mwalimu huyo anasimulia pindi wakiona dalili za kukosekana hatua sahihi, nafasi ya shule hubeba dhamana ya kuishirikisha polisi ili majibu yapatikane na wao kujivisha koti la uzazi wakiwa mashahidi.

Hapo anatoa mfano alikokuwa anafundisha kati ya mwaka 2016 na 2018, kulishawasilishwa polisi matukio manne kwa wanafunzi wenye umri wa miaka kati ya miaka 10 na 13, kukiwapo mkasa wa binti aliyetendewa na mzee wa umri wa babu yake, aliyeishi jirani na shule.

"Mtoto alitueleza kuwa huyo babu alikuwa anampa Sh. 500 na wakati mwingine Sh. 1,000, na alikuwa anakwenda kila siku na mwisho wa siku akazoea. Kesi hizi zote tulizifuatilia mpaka mwisho, kesi hii ya babu ambaye alikuwa mzaliwa wa Pemba, alitoroka na kukimbilia ... ikaishia hewani.

"Hawa wengine ni watoto walikuwa wakifanyiana wao kwa wao, wazazi waliitwa wakakanywa na walipelekwa kupimwa afya zao na baada ya hapo wazazi waliwahamisha shule," anasimulia mwalimu huyo, huku akisisitiza haja ya wazazi kuzidisha ukaribu na watoto wao.

**MKASA WA MJUKUU**

Mratibu wa Kujitolea Kituo cha Watoto cha Msongola Orphanage Trust kilichoko Chanika jijini Dar es Salaam, Mch. Zacharia Maloba, anasimulia moja ya matukio ni la mtoto wa kike wa darasa la tatu (jina linahifadhiwa) ambaye alifanyiwa vitendo vya unajisi wakati akienda kwenye masomo ya ziada (tuition).

Anasema mtoto huyo alifanyiwa madhila hayo wakati akiishi na bibi yake maeneo ya Msongola, baada ya mama yake mzazi kumwacha pamoja na mdogo wake kutokana na vikwazo vya maisha aliyonayo.

"Mama mzazi wa watoto hawa alipowaacha hapo, aliondoka na kwenda kutafuta maisha. Wakati akiendelea na masomo na kutokana na mazingira ya mtaani, bibi aliamua kumwandikisha tuisheni.

"Kwa hiyo mtoto alipokuwa akitoka shuleni badala ya kubaki mtaani, bibi aliamua awe anakwenda kusoma masomo ya ziada kwa mwalimu mmoja.

"Yule mwalimu akaanza kumnajisi mtoto kidogo kidogo, mwishowe mtoto alikuwa akitoka shule moja kwa moja alikuwa anakwenda kwa mwalimu hata kama siyo muda wa masomo," anasimulia.

Mch. Maloba anasema wakati anampokea mtoto huyo ili ahifadhiwe kituoni hapo, kesi ya tukio hilo ilikuwa Kituo cha Polisi Chanika.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima.

"Polisi waliona kwa sababu mtoto huyu alikuwa na mdogo wake na mazingira ya nyumbani kwa bibi siyo salama, waliletwa hapa kituoni kuishi. Kwa hiyo unaona namna ukatili huu ulivyo hatari kwa maisha ya watoto hawa, badala ya kuishi kwenye familia zao wanaishi kituoni," anasimulia.

**ATHARI KISAIKOLOJIA**

Mwanasaikolojia kutoka Hospitali ya Kanda ya Mbeya, Mbuwi Ndagamsu, anasema kesi nyingi wanazokutana nazo hospitalini hapo ni za watu wazima ambao waliwahi kufanyiwa ukatili wakiwa watoto.

"Mtu anakuja analalamika 'ninaumwa kichwa kisichosikia dawa', mwingine analalamika 'mimi ninasahau mambo, ninatamani kujiua muda wote'. Ukimhoji kwa kina unagundua alifanyiwa ukatili akiwa mdogo.

"Bahati mbaya kwa nchi yetu, hawana elimu kuhusu masuala ya saikolojia, mpaka mtu afike hospitalini aambiwe 'kamwone msaikolojia au ashauriwe na daktari', wengi wanakufa na tai shingoni, watu wa namna hii tunaowapokea wana umri unaoanzia miaka 15 hadi 30," anafafanua.

Mwanasaikolojia huyo anasema kesi nyingi huwa ni za ubakaji na manyanyaso ya vipigo kutoka kwa mama wa kambo.

"Juzi (Agosti 13, 2022), nilikuwa na kesi ya binti ambaye alifunga ndoa na ndani ya wiki mbili, akiwa fungate akabakwa na wanaume wanne, nilipomdadisi zaidi akaniambia akiwa mtoto aliwahi kubakwa na wachunga ng'ombe, kesi nyingi zinaumiza, ndiyo maana tunashauri watu waendelee kupata elimu ya saikolojia tiba na ya afya ya akili.

"Kuna watu wanapata magonjwa ya akili, ukimfuatilia kiundani aliwahi kufanyiwa ukatili akiwa mdogo, mwisho wa siku anaishi nao na anafikia umri wa utu uzima anakuwa na tatizo la ugonjwa wa akili," anasema.

**MKATABA KIMATAIFA**

Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto unaoshughulikia haki ya mtoto kote duniani uliopitishwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa Novemba 1989 na kuanza kufanya kazi Septemba 2, mwaka 1990, Tanzania iliukubali Julai 10, 1991, unahimiza ulinzi wa haki za watoto.

Kwa ujumla, haki za mtoto zinazolindwa na mkataba huu zinaweza kugawanywa katika makundi makuu manne, miongoni ni haki ya kuishi kwenye mazingira mazuri ikiwamo kupata lishe bora; haki ya kuendelea, kukua, kupata elimu, haki ya kucheza; haki ya kulindwa na wazazi/walezi/jamii au serikali dhidi ya madhara; na haki ya kushiriki katika masuala yanayomgusa.

Pia ipo Sheria ya Mtoto Na. 21 ya Mwaka 2009 inashughulikia haki za watoto Tanzania ambayo ndani yake zipo haki za mtoto miongoni ni; haki ya kushiriki michezo na shughuli za kiutamaduni, haki ya kulindwa dhidi kudhalilishwa kijinsia na haki ya kuheshimiwa na kuthaminiwa.

Pia sheria hiyo inazungumzia wajibu wa mzazi/mlezi wa kutunza mtoto miongoni ikiwa ni uhuru, haki ya kucheza na kupumzika na elimu na malezi bora.

Katika kipindi cha Januari mpaka Septemba mwaka 2021, ripoti za Jeshi la Polisi nchini zinaonyesha watoto 6,168 kati yao, wasichana ni 5,287 na wavulana 88, wamefanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Kati ya watoto hao, 3,524 walibakwa, 637 walilawitiwa, 1,887 walipata mimba na 130 walichomwa moto baada kuchukua kitu nyumbani.

Kati ya visa hivyo, watuhumiwa waliofikishwa mahakamani ni 3,800 tu, kesi zilizofanyiwa upelelezi ni 2,368 na zilizotolewa hukumu ni 88.

Wakili wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) William Maduhu, anakiri kuwa ukatili wa watoto ni tatizo kubwa licha ya kwamba kuna sheria na Tanzania ni mwanachama wa mkataba wa kimataifa wa kulinda mtoto.

"Serikali imezindua miongozo miwili, moja wa kushughulika na kesi za watoto na mwingine ni wa kushughulikia malezi ya watoto, hii inaonyesha kwamba serikali imegundua kuna shida," anasema.

Maduhu anasema ripoti zinaonyesha ukatili wa watoto kwa mwaka 2020/21, ulikuwa mkubwa na ulichochewa na imani za kishirikina.

Suala lingine analitaja ni maofisa ustawi wa jamii kuwa wachache na kwamba hata waliopo baadhi hawana vitendea kazi yakiwamo magari ya kuwafikisha maeneo ya matukio.

"Tunaishauri serikali iwawezeshe watu wa ustawi wa jamii, mwaka jana (2021) tuliwafundisha maofisa ustawi wa jamii 153, namna ya kushughulika na masuala ya watoto na malezi, hawa wakiwezeshwa maana yake watasaidia kwa kiwango kikubwa kuielimisha jamii dhidi ya ukatili wa kijinsia.

"Sheria yetu ina kamati ya ulinzi wa mtoto kila kata na kila mtaa, huu ni muda mwafaka wa kamati zile, serikali iziwezeshe ziwe na nguvu na zifanye kazi, kupunguza matukio ndani ya jamii," anashauri.

Maduhu anaikumbusha jamii kuwa kosa la ulawiti na ubakaji mtu anapokutwa na hatia huhukumiwa kifungo cha miaka 30 jela na cha juu zaidi ni kifungo cha maisha.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, anabainisha kuwa wizara katika kukabiliana na matatizo hayo, imeendelea kuelimisha jamii na baadhi ya wananchi wameelewa na kuhamasika kuhusu ukatili dhidi ya watoto.

"Wizara imeunga mkono kampeni ya Shujaa wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii Tanzania (SMAUJATA) kwenye mikoa 26 ya Tanzania, kampeni inaratibiwa na kusimamiwa na wizara ikishirikiana na wadau mpaka sasa wananchi 8,319 wamejiunga nayo.

# Gari la Magereza ladaiwa chanzo kifo mkazi wa jiji

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKAZI wa Miyuji jijini Dodoma, Richard Bukombe maarufu Baba Paroko amefariki dunia katika kinachodaiwa na ndugu zake kwamba ni kugongwa na gari ambalo ni mali ya Jeshi la Magereza.

Ndugu zake wamedai kuwa baada ya kumgonga, mwili wake umetelezwa katika chumba cha kuhifadhi maiti cha Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma.

Mdogo wa marehemu, Bulole Bukombe, akizungumza na waandishi wa habari kwa niaba ya familia jana jijini hapo, alisema wanaiomba Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kulifuatilia suala hilo na kuwapa majibu ili wauzike mwili wa ndugu yao.

Bukombe alidai kuwa ndugu yao aligongwa na gari hilo aina ya Land Cruzer Pick Up Septemba 13, mwaka huu, jirani na eneo la hoteli ya Twiga, Msalato jijini hapo majira ya saa 12:30 jioni na kwamba baadhi ya askari wa jeshi hilo, baada ya ajali, walimchukua na kuondoka naye.

"Tumepata taarifa kuwa baada ya kugongwa na kuchukuliwa na watu wa magereza, ikabidi mtoto wa marehemu usiku wa Septemba 13 aende kufuatilia katika maeneo mbalimbali na alipofika katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, aliuliza mapokezi, hakupata taarifa zake.

"Hata hivyo, alipokwenda katika chumba cha kuhifadhi maiti, aliukuta mwili wa baba yake ukiwa umeandikwa "unknown" (mtu asiyefahamika) ndipo akamweleza mtoa huduma kuwa yule ni baba yake na hapo ndipo mwili ukaandikwa jina lake," alidai.

Aliendelea kusimulia kuwa baada ya tukio hilo kutokea, yeye pamoja na wenzake walipatiwa taarifa na mtoto wa marehemu kuwa kaka yao amegongwa na gari na mwili wake umekutwa kwenye chumba cha kuhifadhi maiti ukiwa umetelekezwa.

"Mimi nilikuwa Kaliua na mwenzangu alikuwa Kibaha, tulipigiana simu kuhusu tukio hili na kuja kufuatilia. Tulianzia polisi, hatukukuta taarifa yoyote kuhusu marehemu.

"Hospitalini kitabu cha mapokezi tuliangalia taarifa za Septemba 13 hadi 15 hatukuzipata taarifa za kupokewa kwa ndugu yetu. Tuliulizia kwa mhudumu wa chumba cha maiti, akasema kuwa ndugu yetu aliletwa na watu wa Jeshi la Magereza," alidai.

Kutokana na hali hiyo, alisema familia inachokitaka kwa sasa ni Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuwapatia majibu ili kuiondolea familia sintofahamu iliyotanda.

"Kama Magereza walimpeleka ndugu yetu katika hospitali hii, kwanini wanaficha utambulisho wao? Na hali hii inatufanya sisi familia kuamini kuwa ndugu yetu kifo chake wao wanahusika nacho.

"Hakuna ripoti yoyote iliyotolewa na daktari wa kifo cha ndugu yetu wala cheti cha uthibitisho wa kifo cha ndugu yetu, hivyo tunaomba majibu ya maswali yetu ili tuweze kuuchukua mwili wa ndugu yetu kwa ajili ya maziko," alisema.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, Dk. Ernest Ibenzi, alikiri kuwapo mwili huo katika chumba cha kuhifadhi maiti cha hospitali hiyo, lakini hakuna taarifa zozote za kupokewa kwake.

"Kweli mwili huu upo hapa lakini hakuna taarifa zozote ambazo zinaonyesha kuwa ulipokewa hapa. Huu ni uzembe wa watu waliokuwapo wakati mwili wa marehemu ukiletwa hapa," alisema.

Mkuu wa Gereza la Msalato jijini hapo, alipoulizwa kuhusu tukio hilo, alikiri kuwa analifahamu kama ambavyo watu wengine walivyolisikia lakini akasisitiza kuwa watu wa kulitolea ufafanuzi ni Makao Makuu ya Jeshi la Magereza.

"Watu ambao wanaweza kulielezea suala hili vizuri ni watu wa makao makuu, mimi ninalifahamu kama ambavyo wewe unalifahamu, hivyo makao makuu ndiyo wanaweza kukupa hadithi yote ya suala hilo," alisema Mwambije.



Askari wakitoa elimu ya usalama barabarani kwa madereva wa bodaboda wa mjini Misungwi mkoani Mwanza juzi, kwa ajili ya usalama wao na wa abiria. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mtoto alivyookolewa katika uvungu wa basi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MTOTO wa kike mwenye umri wa miaka 13 amenusurika kifo baada ya kuokolewa na wasamaria wakati akisafiri kutokea mkoani Kagera kwenda Dar er Salaam kwa mama yake mzazi anayeishi Tabata jijini huko akiwa amejificha chini ya uvungu wa basi.

Tukio hilo lilitokea Septemba 13 majira ya saa saba mchana wakati basi lilipanda kutokea mkoani Kagera Kampuni ya Frester lenye namba za usajili T 244 DWF likifanyiwa ukaguzi na mafundi baada ya kufika wilayani Kahama mkoani Shinyanga.

Akisimulia tukio hilo lilivyotokea, Ofisa Ustawi wa Jamii Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Abrahamani Nuru alisema mtoto huyo alikuwa anatokea Kijiji cha Kagya kwa baba yake mzazi aliyefahamika kwa jina moja la Godfrey akielekea kwa mama yake mzazi aliyedai anaitwa Julietha Tofilo.

Alisema kuwa baada ya kuokolewa na mafundi, walimkabidhi katika ofisini za ustawi wa jamii kwa ajili ya taratibu zingine ikiwamo kuwatafuta ndugu zake na hadi jana walikuwa hawajapatikana na alikuwa anaendelea kupatiwa huduma kwa kuwa hali yake kiafya haikuwa nzuri.

Nuru alisema kuwa wakati wa mahojiano, mtoto huyo alikiri alikuwa mwanafunzi wa Shule ya Msingi Kagya mkoani Kagera na aliishia darasa la pili mwaka 2019 na aliamua kutoroka nyumbani kwenda kwa mama yake Tabata jijini Dar es Salaam.

Mmoja wa abiria, Siliveri Samwel alisema alishangaa kuona mtoto huyo akitolewa chini ya uvungu wa gari na mafundi wakati wa ukaguzi kwani kutoka Bukoba mkoani Kagera hadi Kahama ni kilometa 292 na barabara waliyopita ina shida nyingi na wasingebainika mapema, angepoteza maisha kwa kukanyagwa na gari.

Mkuu wa Kitengo cha Usalama Barabarani Manispaa ya Kahama, Flora Nangawe aliwaomba madereva wa mabasi kufanya ukaguzi kwa kushirikiana na mafundi wao ili kuzuia matukio ya watoto wadogo wanaotumia mbinu hiyo kusafiri kwa kujificha chini ya magari na kuhatarisha usalama wao.

Pia aliwataka wazazi na walezi kuwa makini na watoto wao katika malezi ambayo yatawasaidia kutokuingia katika makundi mabaya wakiwa umri mdogo yanahatarisha makuzi yao na baadaye ukubwani kuwa tishio katika jamii.

# Jela miaka 30 kwa kupora na kujeruhi

**Na Samson Chacha,** TARIME

MAHAKAMA ya Wilaya ya Tarime imewahukumu wakazi wawili wa Kijiji cha Gwitiryo kwenda jela kutumikia kifungo cha miaka 30 baada ya kukutwa na hatia ya kumvamia, kumjeruhi na kumpora fedha jirani yao.

Wakazi hao ni Chacha Getarenge na Jacob Saimon, ambao walikuwa wakituhumiwa kutekeleza kosa hilo dhidi ya Charles Ryoba.

Wakisomewa hukumu hiyo katika kesi ya jinai namba 301/2021 na Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Tarime, Yohana Myombo, wawili hao walikuwa wakituhumiwa kumnyang'anya Ryoba Sh. 83,000.

Mwendesha Mashtaka wa Jeshi la Polisi, Inspekta Mhina Komba alidai kuwa watuhumiwa hao wote ni wakazi wa Kijiji cha Gwitiryo, Tarafa ya Inchugu wilayani Tarime.

Alidai watuhumiwa hao kwa pamoja usiku wa Januari 30, mwaka huu, wakiwa na silaha za jadi, walimvamia Ryoba nyakati za usiku, kumjeruhi kwa kumkata na mapanga kichwani na mikononi wakati akirejea nyumbani kwake.

Katika shauri hilo, upande wa mashtaka uliongozwa na Inspekta Mhina, ulileta mashahidi wanne akiwamo mwathirika, daktari aliyemtibu, kibali cha matibabu kilichotolewa na Jeshi la Polisi (PF3) na askari wa upelelezi.

Washtakiwa walijitetea mwenyewe pasi na kuwa na mashahidi wengine.

Inspekta Mhina aliiomba mahakama hiyo kutoa adhabu kali kwa watuhumiwa kwa sababu vitendo vya uhalifu, ikiwamo watu kukatwa mapanga, vimekuwa vikitokea mara kwa mara katika wilaya za Tarime na Rorya.

Akisoma hukumu ya kesi hiyo, Hakimu Myombo alisema: "Kulingana na ushahidi uliotolewa bila ya kuacha shaka yoyote, watuhumiwa wote kwa pamoja ninawatia hatiani kila mmoja kwenda jela miaka 30 ili iwe fundisho kwa watu wengine wenye tabia ya kuwadhuru watu wengine na

kuwapora mali na kuwasababishia ulemavu wa kudumu".

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TAKUKURU mulikeni ahadi za mil. 20/- ili Simba ifungwe

**LIGI** Kuu Tanzania Bara imeanza kwa ushindani mkubwa msimu huu kila timu ikionyesha dhamira yake ya kuvuna pointi katika raundi hizi za mwanzo wakati huu ambao wiki hii inaingia raundi ya tano, huku Yanga ikiwa kileleni kwa idadi tu ya mabao kutokana na kuwa na pointi 10 sawa na Simba na Namungo FC.

Tofauti na msimu uliopita, msimu huu klabu zimewekeza zaidi kwani hata zile ambazo zilizozoeleka kwa kutokuwa na utamaduni wa kusajili wachezaji kutoka nje kama Klabu ya Tanzania Prisons na zingine, na zenyewe zimevuka mipaka ya nchi kufanya usajili.

Hii inaonyesha ni kwa namna gani kila timu ilivyodhamiria kufanya makubwa katika mbio hizo ubingwa wa ligi hiyo, ambayo msimu huu bonasi pamoja na zawadi zitaongezeka kutoka kwa wadhamini wa haki za matangazo, Kampuni ya Azam Media, lakini kuwania kukata tiketi ya michuano ya kimataifa kwa ngazi ya klabu.

Hata hivyo, wakati mbio hizo zikiendelea kumezuka ahadi kwa timu mbalimbali kuahidiwa Sh. milioni 20 kama zitaifunga Simba na zikitoka sare Sh. milioni 10, zawadi ambazo tunazitilia mashaka na tunaona ipo haja ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), kuzimulika zisije kuwa chanzo cha upangaji matokeo.

Kinachotufanya kutilia hofu ahadi hizi ni kwanza, kwa nini zimekuwa zikitolewa kwa timu kutakiwa kuifunga Simba pekee na si zikicheza timu nyingine katika ligi hiyo?

Ikumbukwe ahadi hizi zilianza tangu msimu uliomalizika ambao Klabu ya Yanga ilitwaa ubingwa baada ya Simba kuubeba kwa misimu minne mfululizo, jambo ambalo limeanza tena kwa timu zinazocheza dhidi ya Simba. Kwa kukumbusha tu katika mchezo wa kwanza wa Simba msimu wa 2021/22, wakati ikicheza ugenini dhidi ya Biashara United na mchezo kumalizika kwa sare tasa Septemba 28, 2021, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Mara, Ally Hapi, aliahidi kuipa timu hiyo Sh. milioni 20 endapo itaifunga Simba na Sh. milioni 10 ikipata sare.

Ahadi kama hiyo pia ilitolewa kwa Dodoma Jiji FC na Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, kabla ya timu hiyo kuchezea kichapo cha bao 1-0 dhidi ya Simba kwenye Uwanja wa Jamhuri Oktoba Mosi, 2021.

Kama ilivyokuwa msimu uliomalizika kwa mechi hizo mbili za mwanzo, ambazo wadau na mashabiki walianza kupaza sauti na kuhoji kwa nini iwe dhidi ya Simba, na baadaye kimya cha ahadi za wazi kikatawala huku kukiwa na madai kwamba ziliendelea kutolewa kimya kimya, msimu huu tena zimeanza kusikika.

Katika mchezo wa kwanza msimu huu kwa Simba uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Agosti 17, mwaka huu kabla ya kushinda mabao 3-0 dhidi ya Geita Gold FC, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Geita, Zahara Muhidin Michuzi, aliiahidi kuipa timu hiyo Sh. milioni 20 ikishinda na ikitoka sare Sh. milioni 10.

Kadhalika, siku moja tu baada ya kuingia mkataba wa kuidhamini Tanzania Prisons, Kampuni ya usafirishaji mizigo kwa njia ya bahari ya Silent Ocean, nayo ikatoa ahadi kama hiyo kwa klabu hiyo dhidi ya Simba ambayo iliibuka na ushindi wa bao 1-0 katika Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya Septemba 14, mwaka huu. Kwa ujumla Nipashe tunapenda kuona ahadi kama hizi zikizidi kutolewa kwa timu ama kwa wachezaji ili kuongeza ushindani na ligi yetu kuzidi kuwa bora zaidi, lakini hofu na mashaka yetu kwa nini zinatolewa dhidi ya timu inayocheza na Simba pekee na isiwe dhidi ya zinazocheza na Yanga, Azam, Namungo, Mtibwa na nyinginezo?

Hofu yetu kubwa kusije kukawa na viongozi wa timu kubwa ambazo zinaihofia Simba katika mbio za kutwaa ubingwa hivyo kuwatumia viongozi hao katika kuhakikisha wapinzani wao hawapati matokeo, na kwa njia hiyo inafahamika wazi huo ni upangaji wa matokeo jambo ambalo ni haramu na najisi kubwa katika soka duniani na ambalo litachafua ukuaji wa ligi yetu na soka la Tanzania kwa ujumla.

Hiivyo, tunaiomba TAKUKURU, kwa kutumia mkono wake mrefu, kumulika uhalali wa ahadi hizi ili kulinusuru soka letu lisitumbukie katika tuhumu za upangaji wa matokeo, lakini wawakilishi halali wanaoweza kuleta mafanikio chanya kwenye michuano ya kimataifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

### Waamuzi wafanyie kazi ushauri wa Bodi ya Ligi

**AKIZUNGUMZA** na Kamati ya Waamuzi jijini Dar es Salaam, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi (TPLB), Almasi Kasongo, alisema baadhi ya waamuzi wanaochezesha mechi za Ligi Kuu wana mapungufu ya vitu kadhaa ambavyo kama wakijirekebisha watakuwa ni bora na wala hawatokuwa wakizungumzwa na kulaumiwa mara kwa mara.

Kwa niaba ya Bodi ya Ligi, Kasongo akakumbusha kuwa ili mwamuzi awe bora kuna vitu lazima awe navyo, lakini baadhi yao wanavikosa hivyo kusababisha malalamiko mengi kwenye baadhi ya mechi za Ligi Kuu.

Akazitaja sifa hizo kuwa ni mwendelezo mzuri wa uchezeshaji kwa dakika zote 90 au mechi tofauti, ujasiri, ukosefu wa mawasiliano na mwisho ni akili ya kuzaliwa. Alisema malalamiko mengi yanayojitokeza kwenye mechi mbalimbali ni mapungufu ya vitu hivyo alivyoviainisha.

"Mwamuzi ni kama hakimu au jaji, ni lazima kwanza uwe jasiri, na mwamuzi mzuri anapimwa kwa vitu kama hivyo.

Kuna baadhi ya waamuzi hapa wamekariri kuwa penalti haitoki dakika ya 94, au dakika ya kwanza, huko ni kukosa ujasiri, penalti inatoka dakika yoyote ile hata 97 na kadi nyekundu inatoka muda wowote ule na anaonyeshwa yeyote yule, usiangalie huyu nani nimwonyeshe au huyu ni staa wa timu unaogopa, unajiuliza nikimpa huyu mwezi mzima nitakuwa na amani kweli, unatakiwa utoe bila kujali ni nani, hivyo ni sifa ya ujasiri anayotakiwa kuwa nayo mwamuzi," akasema Kasongo.

Ni kweli kabisa alichokisema Kasongo hapa. Kumekuwa na tabia ya baadhi ya waamuzi wa kizazi hiki kutoa maamuzi hasa kwa timu kubwa zenye mashabiki wengi hususan wa timu za Simba na Yanga.

Wengi wa waamuzi wanaweza kutoa kadi nyekundu au penalti dhahiri kwa timu zinazoitwa au kujiita ndogo, lakini inakuwa ngumu sana kufanya hivyo inapotokea kosa limefanyika kwa timu hizo mbili.

Hii tabia huwa inawapa nguvu baadhi ya viongozi wa Azam FC kudai kuwa kuna maeneo huwa hawatendewi haki, au hawapati faida ya makosa ya kibinadamu kama inavyokuwa kwa timu za Simba na Yanga.

Wanadai makosa mengi ya kibinadamu ya waamuzi hulalia kwa timu yao na timu zingine, lakini huwezi kukuta kwa vigogo hao, ndiyo maana wanaukosa ubingwa.

Mwamuzi anayeona kufanya maamuzi sahihi kwa kuogopa kuwakera mashabiki, kusemwa kwenye mitandao ya kijamii au kutishiwa hana chembe ya ujasiri, hivyo hafai kuwa mwamuzi kwa kuwa atakuwa akizipa adhabu timu dhaifu tu zisizokuwa na uwezo wa kusema au kwa kusemea.

"Kwenye vikao vya kamati hakuna timu ambayo haijapigwa faini kwa mashabiki wake kurusha chupa na mawe, tumefuatilia msingi wake, imegundulika kuwa waamuzi wanakosa muendelezo mzuri wa uchezeshaji na maamuzi. Kosa hilo hilo linafanywa na timu A anaonya, likifanywa na timu B anatoa njano, lingine likifanywa na timu A anatoa njano, lakini hilo hilo likifanywa na timu B anatoa nyekundu.

"Unawafanya mashabiki kuwa na hasira kwa sababu wapo uwanjani na wanaona matukio yote unavyoamua, kwa nini kosa moja utoe maamuzi tofauti kwa timu hii na hii? Akahoji Ofisa Mtendaji Mkuu huyo."

Hapa ukiangalia ni kwamba msingi wake ni mmoja tu. Ule ule wa kutokuwa na ujasiri. Mchezaji wa Simba akifanya kosa ataonywa, hilo hilo akifanya wa KMC atapewa njano, kuna kosa akifanya wa Yanga anapewa kadi ya njano, lakini linafanana hivyo hivyo, wa Dodoma Jiji atapewa nyekundu. Ni woga ule ule aliosema Kasongo ndiyo unasababisha kutokuwa na mwendelezo mzuri wa uchezeshaji.

Mbali na kutumia akili ya kuzaliwa, Kasongo alibainisha kuwa kuna kesi za waamuzi wanaopelekwa kwenye kamati, lakini ukiziangalia unakuta tatizo ni dogo tu, kutokuwa na mawasiliano.

Ni kweli, mawasiliano ni kitu muhimu sana kwenye nyanja yoyote ile, hata kwenye ngazi ya familia tu. Kuna makosa utayaona mwamuzi msaidizi anatakiwa kumsaidia mwamuzi lakini wa kati yeye 'anauchuna' tu na kumwachia kazi kubwa mwenzake kiasi kwamba likitokea tatizo yeye anakuwa kama vile amejiondoa kwenye lawama.

Mwamuzi wa kati na wasaidizi wake wanatakiwa wawe na mawasiliano, huku maeneo yote ambao msaidizi anayatazama awe tayari kumsaidia mwenzake ili kumrahisishia kazi.

Ni baadhi ya waamuzi wasaidizi wachache tu wakiongozwa na Frank Komba na Janeth Balama mara kwa mara ameonekana kufanya kazi kubwa ya kuwasaidia waamuzi kwenye maeneo ambayo wao si rahisi kung'amua, na wamekuwa wakiifanya kwa usahihi mkubwa.

Hawa wanasababisha waamuzi kuchezesha wakiwa hawana presha kwa sababu wanajua wana wasaidizi wazuri na si wa kunyoosha tu kibendera mpira ukitoka, au kuwekwa kona.

Nadhani imefika wakati alichokiona Ofisa Mtendaji Mkuu wa TPLB kwa niaba ya Bodi ya Ligi kifanyiwe kazi na waamuzi wote wa Ligi Kuu Tanzania Bara ili kuondoa malalamiko yasiyo ya lazima.

# CHADEMA, wadau siasa wakumbusha katiba mpya

**Na Jenifer Gilla**

WADAU wa siasa wamesema mwelekeo wa demokrasia nchini uko katika hatua nzuri kutokana na utashi uliopo wa kupata katiba mpya.

Pia wamesema kufungiwa kwa mikutano ya vyama vya siasa nchini ni kikwazo kwa ukuaji wa demokrasia nchini.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti kuhusu Wiki ya Demokrasia Duniani iliyoadhimishwa mwishoni mwa wiki, wadau hao walisema ni lazima marekebisho ya sheria yafanyike na kuwa na katiba mpya inayoendana na mazingira ya sasa.

Mchambuzi wa Siasa, Gwadumi Mwakatobe, alisema demokrasia ya nchi kwa sasa inaelekea kuzuri kwa kuwa ipo katika mchakato wa kuanza kupata katiba ya kidemokrasia ambayo ni mwongozo unaotokana na uamuzi wa wananchi.

Alisema msingi wa kidemokrasia ni kuheshimu uamuzi wa wananchi, hata kama viongozi walio madarakani hawatoupenda.

Alisema Tanzania haijafikia kuwa na demokrasia kamili kwa kuwa katiba iliyopo siyo ya mfumo wa vyama vingi, bali ilitokana na katiba ya chama mwaka 1977 na kuongezwa kipengele cha vyama vingi mwaka 1992.

"Mwaka 1977 hatukuwa na vyama vingi na ninakumbuka hata waliotunga katiba ya chama walikuwa watu 20 tu, akiwamo Pius Msekwa (aliyekuwa Spika wa Bunge 1994-2005). Na hawakuzunguka nchi nzima kukusanya maoni kama inavyofanyika sasa," alisema Gwandumi.

Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mnyika, alisema Tanzania haijakomaa kidemokrasia kutokana na baadhi ya mambo yanaoendelea nchini, ikiwamo kufungia mikutano ya hadhara.

"Kwanza, serikali inatakiwa iondoe zuio la mikutano ya hadhara bila kusubiri kikosi kazi au mabadiliko ya sheria wala kanuni kwa kuwa Sheria ya Vyama vya Siasa na Jeshi la Polisi vinatoa haki kwa vyama kufanya mikutano," alisema.

Mnyika aliongeza kuwa demokrasia ya nchi inaathiriwa na kutokuwapo uchaguzi huru na haki, tume huru ya uchaguzi na uchaguzi wa kisiasa, jambo ambalo mwaka 1991 Tume ya Jaji Francis Nyalali ilipendekeza kuandikwe katiba mpya inayoeleza kuwapo mfumo wa vyama vingi ili mambo hayo yawapo.

"Ili tujenge misingi imara ya kidemokrasia na taasisi imara, hatuna budi tuharakishe kuandika katiba mpya. Kwa kuwa siku ya kidemokrasia imepita siku chache zilizopita, serikali itoe kauli juu ya katiba, kauli ya kukamilisha mchakato wa katiba na waeleze ni lini utatungwa muswada wa sheria ya kurejesha mchakato wa katiba mpya, ili ukamilike kwa wakati kabla ya uchaguzi wa mwaka 2025," alisema Mnyika.

Mchambuzi wa siasa, Dk. Azavel Lwaitama, alisema ili nchi iwe na misingi ya kidemokrasia, uamuzi juu ya maisha ya watu unapaswa utolewe na wananchi wenyewe, jambo ambalo halijafanikiwa nchini.

"Kwa Tanzania upungufu mkubwa ni hilo la kukosekana ugatuzi wa mamlaka. Kama mtu anajiita mkuu wa mkoa, basi ukuu wake utokane na kuchaguliwa kwa utaratibu fulani. Huwezi kusema kuna demokrasia halafu mtu ambaye anashikilia maisha ya watu hajachaguliwa na watu," alisema.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, akizungumza kwa njia ya video wakati wa kuadhimisha siku hiyo, aliyataka mataifa kudumisha demokrasia na kutilia mkazo umuhimu wa uhuru wa vyombo vya habari.

"Lakini kote ulimwenguni demokrasia inarudi nyuma. Raia hawashirikishwi, kutoaminiana na taarifa potofu zinaongezeka. Taasisi za kidemokrasia zinadhoofishwa.

"Sasa ni wa wakati wa kuzungumza, sasa ni wakati wa kusimama na demokrasia, maendeleo na kutetea haki za binadamu. Vyote hivyo vinategemeana na vinahitaji kuimarishwa," alisema.

Septemba 15 mwaka huu, Tanzania iliungana na nchi zingine ulimwenguni kuadhimisha miaka 15 ya siku ya kimataifa ya demokrasia iliyopitishwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mwaka 2007 kuhimiza serikali duniani kuimarisha demokrasia.




Mkurugenzi wa Wateja Wakubwa na Shughuli za Serikali wa NBC, James Meitaron, akizungumza na washiriki wa mkutano wa asubuhi 'Power breakfast business meeting' ulioandaliwa na benki hiyo ili kujadili fursa za biashara, kutambulisha huduma mpya sambamba na kuwajengea uelewa zaidi wateja hao kuhusu faida na manufaa ya huduma hizo, mwishoni mwa wiki jijini Arusha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Baba kortini tuhuma kumnajisi mwanawe

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKAZI wa Kata ya Jamhuri, Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, Saidi Manduta (49), amefikishwa Mahakama ya Hakimu Mkazi ya mkoa huo, akikabiliwa na shtaka la kumnajisi mwanawe wa kumzaa mwenye umri wa miaka 14 anayesoma darasa la tano.

Manduta alifikishwa mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Mwandamizi wa Mahakama hiyo, Conslata Singano. Akisomewa shtaka linalomkabiri na Mwanasheria wa Serikali, Godfrey Mramba, alidai mshtakiwa alitekeleza unyama huo kwa mtoto wake siku tofauti mwezi Agosti, mwaka huu.

Mramba alidai kukamatwa kwa mshtakiwa huyo kumetokana na Jeshi la Polisi kupata taarifa ya mshtakiwa kushiriki kitendo hicho kutoka kwa wasiri wao.

Alidai, askari polisi walifanya upelelezi ikiwa ni pamoja na kumuhoji mtoto na kupata ushahidi wa kutosha uliowezesha kumkamata mshtakiwa na kumfikisha mahakamani.

Kosa linalomkabili mshtakiwa huyo liko chini ya Sheria ya Jinai, kifungu cha sheria 158 (1) (a) kanuni ya adhabu sura ya 16 rejeo la mwaka 2019.

Mshtakiwa amekana kosa na kupelekwa mahabusu hadi Septemba 28, mwaka huu, baada ya upande wa mashtaka kuzuia dhamana.

# Jela miaka 30 kwa kukutwa na bangi

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKAZI wa Tandika wilayani Temeke mkoani Dar es Salaam, Hadija Chikundi (31) amehukumiwa kwenda jela kutumikia kifungo cha miaka 30 baada ya kukutwa na hatia ya kusafirisha dawa za kulevya aina ya bangi kilo 13.7.

Hukumu hiyo iliyolewa na Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama ya Wilaya ya Lindi, Muyonga Magara baada ya kuridhishwa na ushahidi uliotolewa na mashahidi watano, ikiwamo ripoti ya Mkemia Mkuu wa Serikali Kanda ya Mtwara.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Magara alisema: "Ripoti ya Mkemia Mkuu kutoka Mtwara imeeleza bayana madhara ya dawa ya kulevya ya aina ya bangi, inaharibu nguvukazi ya taifa".

Hakimu Magara akitoa hukumu ya kesi hiyo namba 07/2022, kupitia kifungu cha 15 'A' (1) na (2) C Sheria, Sura ya 95, marejeo la mwaka 2019, alisema: "Sheria imenifunga mikono, hivyo ninakuhukumu kwenda jela miaka 30".

Awali ilidaiwa mahakamani huko na Mwanasheria wa Serikali, Mramba kuwa mshtakiwa huyo alikamatwa Februari 27, mwaka huu katika kizuizi cha polisi kilichoko eneo la SIDO, Manispaa ya Lindi, akiwa anasafirisha dawa hizo akitokea Nyangao, Halmashauri ya Mtama kwenda mkoani Dar es Salaam.

Kabla ya kutolewa hukumu hiyo, mshtakiwa alipewa nafasi ya kujitetea, akiomba mahakama kutompa adhabu bali imwonee huruma na kumsamehe kwa sababu kosa hilo ametenda kwa mara ya kwanza, pia ni yatima.

Pia alijitetea kwamba ana mtoto mdogo anayemlea peke yake kulikosababishwa na mwenza wake kufariki dunia miaka miwili iliyopita.

Baada ya utetezi huo, Hakimu Magara alimuuliza Mwanasheria wa Serikali, Godfrey Mramba kama anazo kumbukumbu za makosa ya zamani dhidi ya mshtakiwa huyo, akijibu hana na kudai kuwa upande wa Jamhuri hauna pingamizi na kuiomba mahakama hiyo kumpa mshtakiwa adhabu kwa mujibu wa sheria inavyoruhusu.

# Bunge lataka TBA iwe na kiwanda cha kokoto

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu imeutaka Wakala wa Majengo (TBA) kuwa na kiwanda cha kuzalisha kokoto ili kupunguza gharama za utekelezaji wa miradi.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Selemani Kakoso, alitoa agizo hilo jana wakati wa ziara ya kamati yake kutembelea miradi mbalimbali inayotekelezwa na TBA jijini Dodoma.

Alisema TBA ikifanikisha kuwa na kiwanda cha kuzalisha kokoto, itakuwa imepiga hatua kwa kiasi kikubwa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali inayoitekeleza nchini.

"Zingatieni suala la kuwa na kiwanda za kuzalisha kokoto. Mkifanya hivyo, itawasaidia kupunguza gharama za utekelezaji miradi," Kakoso alishauri.

Alisema miradi iliyotembelewa inajumuisha ujenzi wa Ikulu ya Chamwino, ujenzi wa Mji wa Serikali Mtumba na mradi wa ujenzi wa nyumba 3,500 Nzuguni B.

"Tumepata nafasi ya kutembelea miradi inayotekelezwa na TBA na tumeona kazi kubwa inafanyika ikiwamo miradi hiyo, iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji kuanzia eneo la Mji wa Serikali, Nzuguni B pamoja na Ikulu ya Chamwino. Jambo kubwa na zuri miradi hiyo inatekelezwa na vijana wengi wa Kitanzania," alisema.

Kakoso alisema kuwa kutokana na kasi ya utekelezaji wa miradi iliyoko TBA kwa sasa, ni vyema serikali ikauwezesha wakala huo kwa lengo la kuongeza ufanisi na tija kwa kuwa TBA inamiliki viwanja vingi katika maeneo mbalimbali nchini. "Tunaamini serikali ikibeba jukumu la kuiwezesha TBA kwa kuipatia fedha za kuendeleza maeneo wanayoyamiliki, wakala huu utafanya uwekezaji mkubwa kwa kufanya ujenzi wa nyumba za makazi kwa viongozi na watumishi wa umma," alisema.

Kakoso alisema TBA inakabiliwa na vikwazo kadhaa ikiwamo uhaba wa watumishi, hivyo akaishauri serikali kuhakikisha inausaidia wakala huo katika kuongeza kiwango kikubwa cha watumishi ili kuendana na mahitaji ya sasa.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzu (Sekta ya Ujenzi), Godfrey Kasekenya, alisema amepokea maelekezo na mapendekezo ya kamati hiyo na kuahidi kuwa wizara itayafanyia kazi kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa TBA.

Mtendaji Mkuu wa TBA, Daud Kondoro, aliishukuru kamati hiyo kuridhia kufanya ziara ya kutembelea na kukagua miradi inayotekelezwa na wakala na kuahidi kuongeza ubunifu zaidi katika miradi inayotekelezwa nchini.



Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martin Shigella (kulia), akipanda mti na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Geita Gold Mining Limited, Terry Strong mwishoni mwa wiki mjini humo katika uzinduzi wa kampeni ya kuifanya Geita kuwa ya kijani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# GGML, RC wazindua mpango upandaji miti

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

KAMPUNI ya Geita Gold Mining Limited (GGML) kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Geita na Halmashauri ya Mji wa Geita, imezindua mpango wa upandaji miti katika Mji wa Geita na kando ya barabara ya Geita-Mwanza kwa lengo la kuupendezesha na kuufanya mji huo kuwa wa kijani.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi huo kwenye eneo la Bombambili mjini Geita juzi, Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martin Shigella, alitoa wito kwa wananchi wa Geita kujenga hulka ya kupanda miti ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuifanya Geita kuwa ya kijani.

"Ninaipongeza Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML), taasisi za ulinzi na usalama na viongozi wa serikali waliokusanyika hapa kutuunga mkono katika mpango huu.

"Tumekubaliana kutekeleza kazi hii kila mwezi ili kufikia malengo ya kupanda miti katika maeneo mengi zaidi. Tungependa kuona Geita ikibadilika kuwa ya kijani kwa kuwa na bustani na miti ya kisasa na iliyotunzwa vizuri.

"Leo (juzi) tumetembea kilometa tatu na kupanda miti mingi lakini mwezi ujao, tutaenda mbali zaidi kuelekea eneo la Magogo ilipo ofisi yangu na ya Halmashauri ya Mji wa Geita," alisema.

Akizungumza kwa upande wa GGML, Mkurugenzi Mtendaji, Terry Strong alibainisha furaha yao kuwa sehemu ya mpango huo na kuipongeza Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kwa kuja na mpango huo muhimu ambao umekuja wakati mwafaka katika kipindi cha msimu wa mvua.

"Ninaipongeza Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Mkurugenzi wa Mji kwa kuja na mpango huu. AngloGold Ashanti - Geita Gold Mining Limited, tumedhamiria kuhifadhi na kuboresha mazingira kwani hii ni moja ya tunu zetu za msingi," alisema.

Aliongeza kuwa GGML imekuwa ikiendesha kampeni kadhaa za mazingira tangu mwaka 2000 ilipoanza shughuli zake za uchimbaji mkoani Geita.

"Ni vyema kutambua kuwa zaidi ya asilimia 70 ya leseni yetu maalum ya uchimbaji madini ipo ndani ya hifadhi ya msitu wa Geita ambayo inahitaji kupandwa miti mara kwa mara ili kuilinda na kwa maendeleo endelevu ya Tanzania na manufaa ya sasa na vizazi vijavyo.

"Nina matumaini yangu kuwa kupitia shughuli hizo, jamii itaelewa athari za uhifadhi wa mazingira na kuondokana na vitendo vya ukataji miti ambavyo vina madhara makubwa katika maisha yetu ya kila siku," alisema Strong.

## Maambukizi mapya VVU yalivyopungua

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

MAAMBUKIZI mapya ya Virusi vya Ukimwi (VVU) yamepungua nchini kutoka 81,000 hadi kufikia 54,000 kwa mwaka.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS), Dk. Leonard Maboko, alisema hayo juzi baada ya kutembelea kituo cha maarifa Manyoni akiwa na wajumbe wa Bodi ya TACAIDS.

"Mwaka 2017 tulipofanya utafiti tuliona kiwango cha maambukizi mapya ya VVU kilifikia watu 81,000 kwa mwaka walioambukizwa, lakini hadi kufikia 2021 tunakadiria watu 54,000 wanapata maambukizi mapya ya VVU," alisema.

Dk. Maboko alisema katika utafiti unaofanyika kila baada ya miaka minne hadi mitano pia imebainika hata maambukizi ya vifo yamepungua kutoka watu 32,000 waliokuwa wanakufa kwa mwaka na kufikia watu 29,000.

Vile vile, hali ya unyanyapaa kwa watu wanaoishi na VVU imepungua kutoka asilimia 28 mwaka 2013 hadi kufikia asilimia tano.

Alisema malengo ya TACAIDS ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2030 kiwango cha maambukizi mapya ya VVU, vifo na unyanyapaa inakuwa ni asilimia sifuri kwa kuwa Tanzania bila Ukimwi inawezekana.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya TACAIDS, Hedwiga Swai, alisema Kituo cha Maarifa Manyoni kilifunguliwa mwaka 2016 ili kuwalenga madereva wa malori ya masafa marefu waweze kupata huduma ya uhakika ya kupima HIV na kupata dawa za kufubaza VVU (ARV).

Alisema TACAIDS imefanikiwa kuanzisha vituo kama hivyo katika kanda mbalimbali nchini ikiwamo barabara kuu ya Dar es Salaam- Tunduma, Morogoro-Mwanza na mpango uliopo ni kufungua vituo vingi zaidi.

Swai alitoa wito kwa madereva wa malori na wananchi kufika katika vituo hivyo kupima afya zao na kama wapo walioanzishiwa dawa za ARV wakifika hapo watapata.

HABARI KITAIFA

## Utalii wa picha wavutia maelfu

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA) imesema idadi ya watalii wa picha imeendelea kuongezeka na kufikia 158,108 mwaka wa fedha uliopita, hivyo kuiingizia mamlaka fedha nyingi.

Kaimu Kamishna wa Uhifadhi TAWA, Mabula Nyanda, alibainisha hayo juzi alipozungumza na wahariri na waandishi wa habari katika Msitu wa Pande mkoani Dar es Salaam.

Alisema katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya watalii wa picha 158,108 walitembelea katika maeneo yanayosimamiwa na TAWA, ongezeko ambalo alisema ni kubwa kulinganisha na miaka mingine.

Alisema idadi hiyo ni ongezeko la asilimia 76.2 kulinganishwa na watalii wa picha 37,684 waliotembelea katika maeneo yanayosimamiwa na TAWA kwa mwaka 2020/21.

Alisema kutokana na jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na serikali ikiwamo utoaji wa chanjo ya UVIKO-19, utangazaji wa utalii na kuvutia uwekezaji kupitia programu maalum ya Tanzania - The Royal Tour, mwenendo wa utalii wa picha umeanza kuimarika.

Alisema kutokana na shughuli za utalii wa picha na uwindaji, mamlaka imekuwa ikitoa gawio kwa halmashauri za wilaya, vijiji na maeneo ya Jumuiya za Hifadhi ya Wanyamapori (WMA).

Alisema kati ya mwaka 2016/17 na 2021/22, mamlaka ilitoa Sh. bilioni 37.79 kwa wanufaika hao.

Alisema sambamba na hilo, kanuni za uwindaji wa kitalii zinaelekeza kampuni zilizokodishwa vitalu vya uwindaji kuchangia shughuli za maendeleo kwa walau dola za Marekani 5,000 kwa kila kitalu kwa mwaka.

Kuhusu utalii katika eneo la Malikale na Urithi wa Dunia Kilwa Kisiwani, Mabula alisema eneo la Kilwa ni miongoni mwa fursa zilizoainishwa katika Mkakati Endelevu wa Mamlaka.

Alisema kwa kuwa eneo hilo linapakana na Pori la Akiba Selous ambalo linatoa fursa za utalii wa wanyamapori, mamlaka inaendelea kuweka mkazo katika kutangaza huduma hiyo mpya ya utalii wa maeneo ya malikale na fukwe.

"Hii ni pamoja kukamilisha ujenzi wa miundombinu wezeshi ya utalii ikiwamo jengo la mapokezi, hoteli na njia za waenda kwa miguu," alisema.

Aliongeza kuwa TAWA imenunua boti ya kisasa ya utalii ambayo ina uwezo wa kubeba abiria 30 kwa wakati mmoja kwa ajili ya shughuli za utalii katika maeneo ya Malikale la Kilwa Kisiwani na Songo Mnara.

Alisema aina hiyo ya kipekee ya boti inawezesha watalii kuona viumbe bahari wakiwa ndani ya boti hiyo.

Alisema kuwa sambamba na boti, ujenzi wa njia za waenda kwa miguu na ukarabati wa gati ulifanyika.

Alisema katika kuhakikisha kuwa mapato yatokanayo na utalii yanaongezeka, mamlaka imeboresha miundombinu katika maeneo ya utalii kwa kutumia fedha za bajeti ya maendeleo ya mwaka 2021/22 na fedha za mradi wa Ustawi wa Taifa na Mapambana dhidi ya UVIKO-19.

Alitaja miradi iliyotekelezwa kuwa ni ujenzi na ukarabati wa barabara yenye urefu wa kilometa 431.4, kukamilika kwa ukarabati wa kiwanja cha ndege cha Lake Natron na katika Pori la Akiba Maswa na ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Buturi umekamilika kwa asilimia 50.

Alitaja mradi mwingine kuwa ni ujenzi wa mabanda saba ya watalii, kambi sita za utalii, sehemu sita za kufanyia sherehe pamoja na ujenzi wa malango na vituo saba vya kukusanyia mapato.



Ofisa Mawasiliano wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Elizabeth Eusebius, akitoa elimu ya utunzaji wa miundombinu ya maji kwa wakazi wa Kijiji cha Manga, Kata ya Mkata, Wilaya ya Handeni katika mkutano wa wananchi wa kueleza hatua za utekelezaji mradi wa maji Chalinze awamu ya tatu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Polisi: Ramli chonganishi chanzo matukio ya ukatili

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

KAMANDA wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Janeth Magomi, amesema ramli chonganishi zinazofanywa na baadhi ya waganga wa kienyeji, ni chanzo cha kuendelea kuwapo vitendo vya ukatili ndani ya jamii.

Alitoa angalizo hilo jana katika Kata ya Mondo wilayani Kahama wakati wa mkutano uliohudhuriwa na viongozi wa Sungusungu kutoka vijiji vya Sangilwa, Penzi, Mwanzwagi, Mondo na Bumbiti.

Kamanda Magomi aliwataka waganga wa kienyeji kuacha kufanya ramli chonganishi, akitolea mfano tukio lililotokea Ushetu la mzee kuuawa kikatili, kwamba upelelezi ulipofanyika ilibainika chanzo cha mauaji hayo ni imani za kishirikina.

Alisema tangu amekuwa kamanda wa mkoa huo, kwa muda mfupi amekutana na vitendo vingi vya mauaji ya wazee, ubakaji, mimba za utotoni, wivu wa mapenzi na vipigo kwa wanawake.

"Ninachowaomba ninyi Sungusungu ndiyo mpo kwenye jamii, vitendo vya uhalifu vikitokea mripoti mara moja kwenye Jeshi la Polisi kwani siku hizi siyo kama zamani kwamba polisi wanaogopwa, tuna polisi jamii kila kata, hivyo fichueni uhalifu ili tuweze kuutokomeza," aliagiza.

Diwani wa Mondo, Peja Kija, alisema vitendo vya ukatili vipo na Sungusungu wamekuwa wakisaidia katika kuhakikisha kunakuwapo ulinzi, lakini nao wakati mwingine wanajichukulia sheria mkononi.

Mtemi wa sungusungu Kata ya Mondo, Pondamali Maziku aliwataka wananchi kutofanya uhalifu, akisisitiza kuwa mila na desturi zao kwa mwananchi anayejihusisha na vitendo vya uhalifu hutengwa.

Pia aliwataka viongozi serikalini kutowafumbia macho wahalifu pindi wanapopata taarifa zao kutoka kwa rai wema.

Alisema kuna tatizo pindi wanapowakamata wahalifu na wanapowapa adhabu na kuwatenga, kuna viongozi wanaoingilia taratibu zao.

Mtemi alisema viongozi hao hutoa maagizo ya kutaka wahalifu waachiwe, lakini wanapokaidi kutekeleza agizo hilo hutishiwa kuwekwa mahabusu na kupewa usumbufu wa mara kwa mara, jambo ambalo linawakatisha tamaa kutekeleza majukumu yao.

Mkazi wa Kijiji cha Mondo, Nestory Mohimu alisema ndugu yake alitoa taarifa za mtuhumiwa wa ujambazi, lakini amekuwa akipata usumbufu wa kufuatwa mara kwa mara, hali inayomwogopesha.

## ...400 wafuzu kozi uganga wa kienyeji

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAGANGA 400 wamefuzu mafunzo ya uganga wa kienyeji katika Chuo cha Uganga Kagongwa kilichoko mji mdogo wa Kagongwa, Manispaa ya Kahama huku wakiaswa kutokujihusisha na vitendo vya ramli chonganishi.

Wahitimu hao kutoka mikoa mbalimbali ikiwamo Simiyu, Shinyanga, Tabora, Katavi na Singida wamefuzu masomo mbalimbali yakiwamo matibabu ya dawa za asili aina ya 'Modesta' pamoja na usomaji wa vitabu vya dini mbalimbali ili kuisaidia jamii kuondokana na magonjwa yanayowasumbua.

Akizungumza wakati wa mahafali ya kwanza ya chuo hicho Mkuu wa Chuo, Nyeshi Ramadhani alisema wahitimu hao wamehitimu kozi tofauti zikiwamo za siku sita, miezi tisa na mwaka mmoja na kupatiwa vyeti vinavyowawezesha kutekeleza majukumu yao ya uganga wa asili.

Vilevile, Ramadhani aliwataka kuhakikisha wanasajiliwa na Baraza la Tiba Asilia na Tiba mbadala ili watambulike na kufanya kazi kwa mujibu wa sheria huku akiiomba serikali kuwapatia vibali wahitimu hao 400 ili watekeleze majukumu yao ipasavyo.

Samweli Sumuni, mhitimu wa mafunzo na mkazi wa Nzega mkoani Tabora, alisema elimu aliyoipata itamwezesha kuisaidia jamii kwa kutibu magonjwa mbalimbali. Mbunge wa Kahama, Jumanne Kishimba aliyekuwa mgeni rasmi katika mahafali hayo, alisema serikali inatambua kazi zinazotekelezwa na waganga wa tiba asili na tiba mbadala na yeye amekuwa mstari wa mbele kuwatetea bungeni ili serikali iendelee kuwatengenezea mazingira rafiki ya kufanya kazi.

"Kama sisi tusipoenzi mila zetu za kuongeza na mizimu, tutaendelea kubaki watumwa ndani ya nchi yetu, niwaondoe wasiwasi serikali inatambua matumizi ya dawa za miti shamba na ndiyo maana kipindi cha UVIKO-19, tulizitumia kujinga na janga hili," alisema.

Kishimba aliwahakikishia wahitimu hao kuwa serikali itawapatia vibali vya kufanya kazi zao na kuwataka kufanya kazi kwa kuzingatia sheria na kutojihusisha na vitendo vya kuichonganisha serikali na wananchi hususani katika ramli chonganishi.

# Barrick yapongezwa kutekeleza sera ya ushirikishwaji wananchi

Na Mwandishi Wetu

KAMISHNA wa Tume ya Madini, Janeth Lekashingo, ameipongeza Kampuni ya Madini ya Barrick kwa kuhakikisha inatekeleza sera ya ushirikishwaji wananchi katika mnyororo wa sekta ya madini (Local Content) kwa lengo la kuwanufaisha Watanzania wanaoishi jirani na migodi yake.

Akifunga semina ya siku mbili iliyohusu ushirikishwaji wananchi katika mnyororo wa sekta ya madini (Local Content) iliyoandaliwa na Twiga Minerals Corporation na kufanyika katika Mgodi wa Dhahabu wa Bulyanhulu, kamishna huyo alisema Barrick ni miongoni mwa kampuni zilizotekeleza sera hiyo kwa vitendo.

Semina hiyo ilihusisha wafanyakazi wa Barrick na tume ambao walitoa mada mbalimbali kuhusiana na uendeshaji wa shughuli za uchimbaji madini nchini kwa kufuata sheria na miongozo ya serikali.

"Ninawapongeza sana kwa kuwa mstari wa mbele katika kutekeleza sera hii kwa vitendo na pia kufanikisha miradi ya maendeleo katika maeneo yanayozunguka migodi yenu kupitia fedha za uwajibikaji katika jamii (CSR)," alisema.

Lekashingo alisema moja ya majukumu ya tume ni kusimamia wadau katika sekta ya madini kuhakikisha wanatekeleza sera hiyo hususani katika utoaji wa zabuni kwa kampuni ya wazawa yaliyosajiliwa na tume hiyo na kampuni za nje zinazoshirikiana na wazawa, ikiwamo suala la kutoa ajira kwa wazawa.

Alisema tume iko tayari kutoa ushauri wa kitaalamu bila malipo kwa Barrick na wadau wengine katika sekta ya madini kuhakikisha sera hiyo inatekelezwa kwa lengo la kuwawezesha Watanzania kunufaika na sekta ya madini.

Akiwasilisha mada ya utendaji wa shughuli za Barrick, Meneja wa kampuni hiyo, Georgia Mutagahywa alisema hadi kufikia sasa, asilimia 70 ya watoa huduma kwenye midogo yake ni Watanzania.

"Kampuni imefanikiwa kutekeleza sera hii kwa vitendo katika maeneo ya ajira, utoaji wa zabuni, sambamba na kuendesha miradi ya kusaidia jamii katika maeneo yanazozunguka migodi yake nchini kupitia fedha zilizotengwa kwa ajili ya kutoa huduma kwa jamii (CSR)," alisema.

Mutagahywa alisema Barrick imeanzisha programu ya kuendeleza wafanyabiashara wa ndani (Local Business Development Programme (LBD) inayosimamiwa na Mgodi wa North Mara, ambayo ni mhimili wa kusimamia kanuni hii na kuhakikisha Watanzania wananufaika nayo kwa asilimia kubwa kwa kuboresha maisha yao kupitia uwekezaji sekta ya madini. Pia wanaelimishwa kuhusu fursa zilizopo kwenye sekta hiyo na tayari baadhi ya wafanyabiashara wamepatiwa mafunzo katika awamu ya kwanza.

Sera ya 'Local content' ilianza kazi mwaka 2017 ikilenga sekta ya madini, mafuta na gesi ili kuhakikisha uchimbaji wa madini na mapato yake yanawanufaisha Watanzania, kwa lengo la kupanua uwanda wa kibiashara na kukuza ajira.



Meneja wa Barrick nchini, Georgia Mutagahywa, akitoa mada katika semina ya ushirikishwaji wananchi kwenye mnyororo wa sekta ya madini iliyofanyika mgodi wa Bulyanhulu mwishoni mwa wiki. Kulia ni Kaimu Meneja Mkuu wa Mgodi wa Barrick Bulyanhulu, Jan Jacobs.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wamiliki maduka dawa watakiwa kuvuta subira

Na Mwandishi Wetu

MWENYEKITI wa Umoja wa Wamiliki Maduka ya Dawa Muhimu (UWAMADAMUDA), Dk. Juma Mganga, amewataka wanachama wa umoja huo kuwa na subira, kufuata sheria, taratibu na kanuni za nchi wakati wanashughulikia tatizo lao la kufanya biashara maeneo ya mjini.

Pia ametaka wanachama na wasio wanachama waungane ili kilio chao kisikike serikalini kwa kuwa umoja wao ndiyo nguzo pekee ya kufanikisha jambo hilo.

Kilio cha wamiliki wa maduka hayo ni kuambiwa wahamie nje ya mji ili mjini yabaki maduka makubwa ya dawa.

Aliyasema hayo katika maadhimisho ya miaka 10 ya umoja huo yaliyofanyika jijini Dar es Salaam na kubainisha matatizo mbalimbali yanayowakumba wanachama hao.

Alisema tatizo kubwa linalowasibu ni kanuni iliyowekwa na Baraza la Wafamasia kuondoa maduka ya dawa muhimu yasikae mjini na kutolewa vibali vya umiliki wa maduka kwa ubaguzi.

"Nawaomba wamiliki wote wa maduka ya dawa tufuate sheria na taratibu za nchi yetu. Ninawaomba mjisajili katika umoja huu ili muweze kutambulika kisheria kama wamiliki wa maduka ya dawa muhimu nchini," alisema Mganga.

Makamu Mwenyekiti wa UWAMADAMUDA, Abdul Mwaijuma, alisema kumekuwapo kundi la wakaguzi feki wanaotumia matatizo yao kama mtaji kwa kutembelea na kuwatapeli.

Katika kupambana na matapeli hao, alisema wanatoa elimu kwa wanachama wao ya kuwatambua ili kuepusha utapeli na udanganyifu.

"Tunahamasisha kuwa umoja ni nguvu, tujiunge, lakini kuwapo kwetu sio tunatetea maovu, asitoke mtu akauza dawa za serikali, akachoma sindano kiholela kwa sababu yupo kwenye umoja, umoja wetu upo kwa ajili ya kutetea haki zetu na kusimamia sheria," alisema Abdul.

Sadati Kihindi, mmiliki wa duka la dawa muhimu alisema umoja huo unawasaidia mambo mbalimbali ikiwamo kutetea watu waliofungiwa maduka.

Pia kuwasaidia kutambuaa dawa mpya za binadamu zinazoingia sokoni, pamoja na kutambua sheria zao kama wanunuzi na wamiliki wa maduka za dawa muhimu.

■**Imeandaliwa na Owen Bariki na Golden Kisapile (TUDARCo)**

## Mradi wa maji Chalinze awamu III wafikia pazuri

Na Joseph Mwendapole

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) imesema utekelezaji wa mradi wa maji Chalinze awamu ya tatu umefikia asilimia 90.

Msimamizi wa mradi huo, Thadei Mwajombe, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki alipozungumza na wakazi wa Kijiji cha Manga na Kimange wilayani Handeni mkoani Tanga.

Alisema mradi huo unajengwa na mkandarasi AFCON na tayari ujenzi wa matenki 18 umekamilika, vioski vimekamilika na vimekabidhiwa pamoja na ujenzi wa mtandao wa mabomba kwa urefu wa kilomita 200 ambao tayari umekamilika.

"Tunatarajia kukamilisha utekelezaji wa mradi huu mwezi Desemba mwaka huu na huduma itaanza kupatikana, hivyo wananchi muwe watulivu wakati mamlaka inakamilisha utekelezaji wa mradi huu," alisema.

Ofisa Mawasiliano DAWASA, Elizabeth Eusebius, aliwataka wanufaika wa mradi huo kuwa waangalifu wa miundombinu ya maji kwa kuepuka kuharibu, kuhujumu na kuingilia ujenzi unaoendelea kwenye maeneo yao ili mkandarasi amalize kazi kwa wakati na wananchi wapate huduma.

"Mradi wa maji Chalinze awamu ya tatu unaendelea kutekelezwa kwa kasi ukihusisha ujenzi wa vioski vya maji kwenye eneo la Manga ambavyo viko katika hatua ya ukamilishwaji ili huduma ianze kupatikana kwa uhakika," alisema.

Elizabeth aliongeza kuwa mamlaka imejikita katika kuhakikisha wananchi wanapata maji, hivyo kila mmoja ana jukumu la kutunza miundombinu ya maji.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Manga, Luhizo Rashid aliishukuru serikali kwa kuwaletea mradi mkubwa na wenye manufaa kwa wananchi wa Chalinze na kuwataka kutoa ushirikiano kwa DAWASA ili mradi ukamilike na maji yapatikane.

Aliwataka wakazi wa Kijiji cha Manga kutoa ushirikiano kwa watekelezaji wa miradi ya maji.

Aliwataka kulinda na kutunza miundombinu ya maji ili mradi ulete manufaa kwa wananchi wengi na kuondokana na shida katika upatikanaji wa majisafi.

Nipashe
Spotika



MAKOCHA 5 WALIOKALIA KUTI KAVU EPL UK. 12-13



HAALAND

# NYOTA 5 WALIOONDOKA NA KUDHOOFISHA TIMU

**LONDON,** England

DIRISHA la uhamisho linaweza kuwa kipindi kigumu sana kwa baadhi ya klabu.

Ni wakati wa kubaini udhaifu wa timu na jambo jingine kabisa kuushughulikia kwa kuleta wachezaji wenye hadhi sahihi. Kuondoka kwa wachezaji ni sababu nyingine kuu ya wasiwasi kwa timu na hii huathiri timu.

Wachezaji hawawezi kulaumiwa kwa kutaka kuchezea klabu kubwa zaidi barani Ulaya au kutaka kujaribu changamoto mpya au kufuata hundi nono ya malipo. Lakini, kujaribu kuhakikisha kuwa kuondoka hakuathiri wimbo wa timu ni kazi ngumu sana.

Wachezaji wengi wakubwa walibadili upande msimu huu wa majira ya joto. Bila kuchelewa zaidi, hebu tuangalie wachezaji watano waliondoka kwenye timu zao ambao wameziacha na udhaifu mkubwa, haya sasa...

### #5. Paulo Dybala - Juventus

Mkataba wa Paulo Dybala na Juventus ulikuwa unamalizika msimu huu wa majira ya joto. Juventus na mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina hawakufikia makubaliano kuhusu suala la mkataba mpya. Kuondoka kulisababishwa zaidi na uamuzi wa 'Bianconeri' hao kukataa ahadi waliyoitoa kwa Dybala Oktoba mwaka jana.

Kwa mujibu wa Fabrizio Romano, Juventus walikuwa wamekubali kumpa Dybala mkataba wa miaka minne wenye thamani ya Euro milioni 8 kwa mwaka. Hata hivyo, Juventus walibadilisha masharti ya mkataba huo na mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina hakufurahishwa na masharti hayo mapya.

Tangu wakati huo, amejiunga na AS Roma kwa uhamisho huru. Kuondoka kwa Dybala bila shaka kumeondoa ubunifu mkubwa kwenye safu ya mashambulizi ya Juventus. 'Kibibi Kizee' hicho kimeanza kampeni mpya kwa kusuasua, kikishinda mechi mbili na sare nne kati ya mechi sita za Serie A hadi sasa.

Pia walianza kampeni yao ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kupoteza 2-1 dhidi ya Paris Saint-Germain.

### #4. Erling Haaland - Borussia Dortmund

Erling Haaland ni mmoja wa washambuliaji bora zaidi duniani akiwa na umri wa miaka 22. Alifunga mabao 86 na kutoa asisti 23 katika mechi 89 katika mashindano yote akiwa na Borussia Dortmund kwa misimu miwili na nusu. Kuondoka kwa mshambuliaji huyo wa kiwango cha juu wa Norway siku zote kungekuwa na athari kubwa kwa Dortmund.

Ili kuendana na Bayern Munich, Dortmund ilihitaji mchezaji wa ubora wa Haaland. Wamepoteza kiungo muhimu na wana uwezekano wa kupoteza mwelekeo katika majaribio yao ya kuendelea kuwa wapinzani wa Bayern kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga.

Wakati huo huo, Haaland ameanza vema maisha ya kule Manchester City. Amefunga mabao 13 na kutoa asisti katika mechi nane kwenye michuano yote kwa upande wa kikosi hicho cha Pep Guardiola hadi sasa.

### #3. Jules Kounde - Sevilla

Sevilla wako nafasi ya 16 kwenye jedwali la Ligi Kuu Hispania, LaLiga, baada ya kucheza kwa wiki sita. Wamechinda mchezo mmoja msimu huu katika LaLiga na kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya walipoteza mchezo wao wa kwanza kwa mabao 4-0 dhidi ya Manchester City.

Safu yao ya ulinzi ni ya kusuasua na inaweza kuhusishwa moja kwa moja na kuwapoteza mabeki wao wa kati chaguo la kwanza, Jules Kounde na Diego Carlos.

Kati ya hao wawili, kuondoka kwa Kounde kwenda Barcelona kunaonekana kuwasumbua zaidi. Sevilla, waliruhusu mchezaji mzuri kama huyo kuondoka kwa kitita cha Euro milioni 55.

### #2. Antonio Rudiger - Chelsea

Mwanzo mbaya wa Chelsea katika msimu mpya umepelekea Thomas Tuchel kutimuliwa kwenye nafasi ya ukocha. Walitumia zaidi ya Euro milioni 180 kuimarisha safu yao ya ulinzi msimu huu wa majira ya joto. Lakini ubora wa safu ya ulinzi umeshuka tu msimu huu na hiyo inazungumza juu ya uwezo wa Antonio Rudiger.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani alikuwa 'mnyama' chini ya Tuchel. Alikuwa na uimara katika safu ya nyuma ya Chelsea na hangewaruhusu washambuliaji kupata muda wa amani katika nafasi ya tatu ya mwisho.

Baada ya kushindwa kufikia makubaliano na Rudiger kuhusu suala la mkataba mpya, Chelsea walilazimika kumtazama akijiunga na Real Madrid kwa uhamisho wa bure. 'The Blues' hao wameruhusu mabao tisa katika mechi zao sita za kwanza za Ligi Kuu msimu huu.

### #1. Sadio Mane - Liverpool

Katika nusu ya kwanza ya msimu wa 2021-22, Sadio Mane alikuwa nje ya kiwango na alionekana kuwa mtu wa kutengwa kabisa. Hata hivyo, alibadilisha mambo kwa kiasi kikubwa katika nusu ya pili ya kampeni na alikuwa katika hali ya juu kwa klabu na nchi tangu wakati huo.

Mane alifunga mabao 23 na kutoa pasi tano za mabao katika mechi 51 katika michuano yote aliyoichezea Liverpool msimu uliopita. Baada ya kupata huduma za Luis Diaz kutoka FC Porto, Januari 2022, Liverpool walihisi kuwa haingeleta tofauti kubwa ikiwa wangemwacha Mane kuondoka msimu wa majira ya joto.

Wamemruhusu na wanaanza kujutia uamuzi huo sasa na wameanza vibaya msimu mpya. Wanakosa makali ambayo Mane alileta kwenye mashambulio na wanaonekana kutokuwa na meno ya kwenda mbele mara kwa mara.

Wakati huohuo, mchezaji huyo wa kimataifa wa Senegal anatamba katika klabu ya Bayern Munich, akiwa amefunga mabao matano katika mechi nane kwenye michuano yote.

## ISIKUPITE

MSHAMBULIAJI mpya wa Liverpool, Darwin Nunez, aliyesajiliwa majira haya ya joto kwa pauni milioni 85 kutoka Benfica ya Ureno, ndiye mchezaji ghali zaidi kuwahi kusajiliwa katika historia ya klabu hiyo.



# MAKOCHA 5 WALIOKALIA KUTI KAVU EPL

**LONDON,** England

TUMEINGIA kwenye wiki ya mechi saba za msimu wa Ligi Kuu ya England (EPL) wa 2022-23 na makocha wawili tayari wamefutwa kazi.

**Scott Parker alitimuliwa na Bournemouth baada ya kuchapwa mabao 9-0 na Liverpool, Agosti 27, mwaka huu.**

Thomas Tuchel alitimuliwa kule Chelsea baada ya kuwa na mwanzo mgumu kwenye Ligi Kuu.

Katika hali fulani, mabadiliko ni suluhisho la wazi, lakini hiyo inaweza isiwe hivyo kila mahali.

Kwa kuzingatia hilo, hebu tuwaangalie makocha watano wa Ligi Kuu England ambao wanaweza kutimuliwa msimu huu, twende sasa...

**#5. Frank Lampard (Everton)**

Kikosi cha Frank Lampard cha Everton (kabla ya mchezo wa jana dhidi ya West Ham United), bado hakijashinda mchezo hata mmoja katika msimu mpya wa Ligi Kuu. Wametoka sare nne na kupoteza mbili hadi sasa. Kocha huyo wa zamani wa Chelsea aliteuliwa kuchukua mikoba ya 'Toffees' hao katikati ya msimu uliopita.

Hajaweza kuiboresha Everton wala kupata matokeo mazuri. Walifanikiwa kwa shida kunusurika kushuka daraja msimu uliopita. Lampard amesimamia mechi 28 katika mashindano yote kama kocha wa Everton. Ameshinda mechi tisa pekee na kupoteza 13.

Iwapo matokeo ya Everton hayataimarika kwa kiasi kikubwa katika kipindi cha miezi michache ijayo, Lampard ana uwezekano mkubwa wa kufutwa kazi.

**#4. Bruno Lage (Wolverhampton Wanderers)**

Wolverhampton Wanderers wameanza vibaya msimu wa Ligi Kuu 2022-23. Wameshinda mchezo mmoja tu kati ya sita hadi sasa na wameshindwa kupata ushindi katika mechi zao tano za kwanza za kampeni mpya. Ushindi huo ulikuja dhidi ya Southampton na ulikuwa wa kwanza kwao tangu Aprili.

Ulikuwa ushindi wa kwanza kwa Wolves katika mechi 13 za Ligi Kuu England. Kikosi hicho kimefunga mabao matatu pekee katika mechi sita za ligi hadi sasa msimu huu. Sasa watacheza na Liverpool na Manchester City katika mechi zao mbili zijazo.

Baada ya suluhu na Bournemouth, Agosti 31 aliwataka mashabiki wao kuwa na subira. Lakini wasipoona dalili chanya zaidi katika wiki zijazo, kwa kweli hawana sababu yoyote ya kubaki na subira.

**#3. Steven Gerrard (Aston Villa)**

Aston Villa wameleta wachezaji wachache wenye ubora ili kumuunga mkono kocha wao Steven Gerrard. Kwa bahati mbaya, hiyo haijatafsiri matokeo kwenye uwanja na shinikizo linaanza kuongezeka kwa Gerrard na wenzake.

Villa wameshinda mechi moja, sare moja na kupoteza nne kati ya sita za kwanza za Ligi Kuu England msimu huu. Kuwashikilia mabingwa watetezi wa Ligi Kuu England, Manchester City kwa sare yalikuwa matokeo mazuri. Lakini Gerrard atasalia tu kazini ikiwa timu yake inaweza kuendeleza uchezaji huo.

Kufikia sasa, nahodha huyo wa zamani wa Liverpool anaonekana kuwa kwenye wakati mgumu.

**#2. Brendan Rodgers (Leicester City)**

Inasikitisha kuona Leicester City wakiwa katika nafasi ya 20 kwenye jedwali la Ligi Kuu baada ya mechi sita. Walikuwa wamejiimarisha kama upande ambao ulikuwa wa nusu ya juu ya jedwali katika misimu kadhaa iliyopita. Lakini wanaonekana kupunguzwa kasi.

Dirisha bovu kabisa la uhamisho limekuwa na madhara kwao. Leicester City waliamua kutotumia fedha nyingi kununua wachezaji wapya msimu huu wa majira ya joto huku Wout Faes aliyesajiliwa kwa pauni milioni 15.3 ndiye mchezaji pekee aliyewagharimu fedha.

Rodgers ameonekana kuchukizwa na ukosefu wa biashara ya uhamisho. Baada ya kufungwa bao 1-0 na Manchester United, alisema (kupitia ESPN):

"Kwa heshima kubwa, hatujapata msaada katika soko ambalo timu hii ilihitaji. Ukiangalia klabu katika ligi tano bora zote zimeongeza wachezaji na sisi hatujaweza kufanya hivyo na imekuwa ngumu kwetu. Tulihitaji msaada na hatujaupata."

Msimu wa Leicester unaelekea kwenye eneo la 'kitu lazima kitoe'. Iwapo hawataweza kuboresha matokeo yao, kuna uwezekano mkubwa wa Rodgers kufukuzwa hivi karibuni.

**#1. Jurgen Klopp (Liverpool)**

Mambo yanaweza kubadilika kwa kupepesa macho katika soka la kisasa. Thomas Tuchel aliiongoza Chelsea kutwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka mmoja uliopita. Alitimuliwa (Septemba 7, mwaka huu) baada ya Chelsea kuanza vibaya kampeni mpya.

Liverpool walikaribia kutwaa mataji manne msimu uliopita, lakini wakashinda Kombe la FA na Kombe la Ligi. Lakini wapo katika msimu wa 2022-23, wakistahimili mwanzo ambao bila shaka umekuwa mbaya zaidi kuliko ule wa Chelsea.

Liverpool wako nafasi ya nane kwenye msimamo wa Ligi Kuu (kabla ya mechi za jana) wakiwa na ushindi mara mbili pekee katika mechi sita za kwanza. Pia walipata kipigo cha aibu cha mabao 4-1 kutoka kwa Napoli katika mechi yao ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Ulaya (Septemba 7).

Mradi wa Klopp wa Borussia Dortmund ulikwama katika mwaka wake wa saba wa kuinoa klabu hiyo. Ndivyo ilivyotokea kule Mainz, ambao walishuka daraja katika msimu wa saba wa Klopp. 'Laana ya msimu wa saba' ya Klopp bado inaonekana kuwa na athari.

Kumtimua Klopp kunaonekana kutowezekana baada ya aina ya uboreshaji wa Liverpool chini yake. Lakini kutokana na hali ya kusisimua ya soka la kisasa, ana nafasi kubwa ya kutimuliwa pale Liverpool.




KLOPP

## Nukuu

"Lewandowski ni mchezaji mahiri. Anajua kuzunguka uwanja. Ninapofungua nafasi, anajua pa kuhamia. Nilipata nafasi ya kuungana naye na Ousmane (Dembele) leo (Jumamosi iliyopita), na ilikuwa nzuri sana," **Mshambuliaji wa Barcelona, Memphis Depay akisifu muunganiko wake na Lewandowski wakati wakishinda 3-0 dhidi ya Elche kwenye La Liga juzi.**



"Cristiano ni mchezaji wa kushangaza, ni shoo kamili ya kumtazama akifunga mabao. Lakini kwangu, Messi amekamilika zaidi, mchezaji ambaye anakupa kila kitu, hivyo kwa ajili yangu, nabaki na Leo Messi," **Nyota wa Barcelona, Pedri akiweka bayana nani aliye bora kwake kati ya Cristiano Ronaldo na Lionel Messi.**



"Kilichoshangaza tu ni idadi ya wachezaji ambao hawachezi soka mara kwa mara katika klabu zao, kutokana na msimamo ambao Gareth (Southgate) alikuwa nao alipopata kazi ya kuchagua wachezaji waliopo kwenye kiwango. Jadon Sancho atakuwa mchezaji mmoja, ambapo tunakiangalia kikosi hicho (cha England) na kufikiria, kikosi hicho ni mengi tungetarajia," **Nguli wa Manchester United, Rio Ferdinand akihoji kutokana na uamuzi wa Gareth kumwacha Jadon Sancho katika kikosi cha England.**






Mfungaji wa bao la kwanza la Yanga, Farid Mussa akimtoka beki wa Zalan FC kwenye mechi ya hatua ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi na wenyeji kushinda 5-0. **MPIGAPICHA WETU**

# USHINDI WA KISHINDO AWALI UNAVYOITESA YANGA CAF

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA wa Tanzania Bara, Yanga, juzi walifanikiwa kutinga raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya kuichapa Zalan FC ya Sudan Kusini jumla ya mabao 5-0 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**Yanga inatinga hatua hiyo kwa jumla ya mabao 9-0, kwani wiki moja iliyopita ilishinda mabao 4-0 kwenye uwanja huo huo.**

Zalan haikucheza mechi yoyote nchini kwao, badala yake iliutumia Uwanja wa Benjamin Mkapa kikanuni kama wa nyumbani Septemba 10 na kupoteza kwa mabao 4-0, kabla ya mechi ya juzi.

Matokeo ya mechi hiyo yameifanya Yanga kutinga raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa baada ya miaka mitano. Mara ya mwisho ilikuwa ni mwaka 2017 ilipoifunga Ngaya Club de Mde ya Comoro kwenye raundi ya awali na kutinga hatua hiyo.

Pia, imeweka rekodi ya kutinga hatua hiyo kwa kutoa vichapo vikali kama ambavyo ilivyokuwa ikifanya huko nyuma. Hii si mara ya kwanza kwa timu hiyo kutinga hatua hiyo kwa kishindo ikitoa adhabu kali kwa timu ilizokutana nazo.

Katika makala haya tumekukusanyia mechi za raundi ya awali ambazo Yanga ilishinda kwa kishindo, ikitinga raundi ya kwanza, haya sasa...

**#1. Yanga 7-2 St. Louis (1992)**

Ni mwaka ambao bado mechi za mabingwa wa Afrika zilikuwa zinatambuliwa kama Klabu Bingwa Afrika. Ilikuwa ni 1992, Yanga ilipoanza raundi ya kwanza kwa kucheza dhidi ya St Louis ya Shelisheli.

Kwenye mechi ya kwanza, Yanga ilikwenda ugenini na kuikung'uta timu hiyo mabao 3-1 na mchezo wa marudiano nchini katika Uwanja wa Taifa (sasa Uhuru), ilishinda tena kwa mabao 4-1. Matokeo ya jumla yakawa mabao 7-2, Yanga ikatoka kwenye hatua ya awali na kutinga raundi ya kwanza.

Hata hivyo, kwenye raundi hiyo ilitolewa kwa jumla ya mabao 3-1 dhidi Ismailia ya Misri. Kwenye mechi ya kwanza nchini, wageni walishinda mabao 2-1 na Yanga ikaenda kukomaa ugenini nchini Misri na kutoka sare ya bao 1-1, ukawa mwisho wao.

**#2. Yanga 14-1 Etoile d'Or (2009)**

Hapa tayari ilianza kuitwa Ligi ya Mabingwa Afrika, Yanga ilicheza dhidi ya Etoile d'Or Mirontsy ya Comoro mwaka 2009. Mechi ya kwanza ilipigwa Uwanja wa Taifa Dar es Salaam (Sasa Mkapa), Yanga ilipata ushindi wa mabao 8-1.

Mkenya Boniface Ambani alipachika mabao manne kwenye mechi hiyo, Jerry Tegete akifunga mawili, Mrisho Ngasa na beki raia wa Malawi Wisdom Ndlovu wakifunga bao moja kila mmoja. Mechi ya marudiano nchini Comoro, Yanga tena ilifanya maangamizi, ikishinda mabao 6-0. Ushindi huo iliifanya kutinga raundi ya kwanza ya ligi hiyo, ambapo ilikutana na Al Ahly ya Misri.

Iliishia kwenye raundi hiyo baada ya kuchapwa mabao 3-0 nchini Misri na kukubali kipigo cha bao 1-0 nchini, hivyo kutolewa kwa jumla ya mabao 4-0.

**#3. Yanga 12-2 Komorozine (2014)**

Yanga ilipata tena karamu ya mabao na kufanikiwa kutinga raundi ya kwanza kutoka ile ya awali mwaka 2014 ilipocheza dhidi ya Komorozine de Domoni ya Comoro. Iliitoa kwa jumla ya mabao 12-2, ikishinda mabao 7-0 nyumbani na ugenini 5-2.

Kwenye mechi ya kwanza, mabao matatu yalifungwa na Mrisho Ngassa, Didier Kavumbagu akifunga mawili, Nadir Haroub Cannavaro na Hamisi Kiiza wakifunga bao moja kila mmoja. Kwenye mechi ya marudiano, yalikuwa tena mabao matatu ya Ngassa 'hat-trick', Hamisi Kiiza na Simom Msuva na kuifanya kutinga kwa mara nyingine tena raundi ya kwanza.

Kwenye mechi ya raundi ya kwanza, Yanga ilicheza dhidi ya Al Ahly ya Misri, kila timu ikishinda bao 1-0 nyumbani, lakini ikatolewa kwa mikwaju ya penalti 4-3.

**#4. Yanga 6-2 Ngaya (2017)**

Yanga ilicheza tena Ligi ya Mabingwa Afrika mwaka 2017 na kufanikiwa kutinga raundi ya kwanza kwa idadi kubwa ya mabao, safari hii zamu ikiwa ya Ngaya Club de Mde ya Comoro.

Kwenye mechi ya kwanza ikichezwa jijini Moroni, Yanga ilishinda mabao 5-1, yaliyofungwa na kiungo Mzambia, Justin Zulu, Simon Msuva, Obrey Chirwa, Amissi Tambwe na Thabani Kamusoko. Mechi ya marudiano, Ngaya ilivimba na kulazimisha sare ya bao 1-1 nchini, Yanga ikasonga mbele raundi ya kwanza kwa ushindi mnono wa mabao 6-2.

Ilishindwa kuvuka hatua inayofuata baada ya kutolewa na Zanaco ya Zambia kwa bao la ugenini, ikitoka sare nchini ya bao 1-1,

**#5. Yanga 9-0 Zalan FC (2022)**

Miaka mitano imepita, kabla ya Yanga kutinga tena kwenye raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika ilipoichakaza Zalan FC ya Sudan Kusini mabao 9-0. Hii ni baada ya msimu uliopita kutolewa dhidi ya Rivers United kwenye hatua za awali za michuano hiyo, ilipofungwa jumla ya mabao 2-0, bao 1-0 kila mechi.

Straika Fiston Mayele alifunga mabao sita kwenye idadi hiyo, kila mechi akipiga 'hat-trick'. Kwenye mechi ya kwanza alifunga mabao matatu, moja likifungwa na Feisal Salum, na mechi ya marudiano Mayele alifunga tena matatu, Stephane Aziz Ki akifunga bao moja na Farid Mussa.

Safari hii kwenye raundi ya kwanza itacheza na mshindi wa jumla kati ya St. George ya Ethiopia au Al Hilal ya Sudan. Je, safari hii itavuka na kutinga makundi kama ilivyofanya mara ya mwisho 1998?

**JE, WAJUA?**



KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, ndiye kocha anayelipwa mshahara mrefu zaidi kwa Ligi Kuu England, akivuta kitita cha pauni milioni 19 kwa mwaka akifuatiwa na Jurgen Klopp wa Liverpool (pauni milioni 16 kwa mwaka) na Antonio Conte wa Tottenham (pauni milioni 15 kwa mwaka).





## Wananchi waomba polisi kuongeza doria

Na Renatha Msungu, DODOMA

WAKATI Jeshi la Polisi limekamata wahalifu 126 wa makosa mbalimbali mkoani hapo, wakazi wa Mtaa wa Relini, Kata ya Kizota wameliomba jeshi hilo kuongeza doria ili kuwanusuru kuvamiwa na watu wasiojulikana ambao walivamia eneo hilo na kujeruhi watu kwa mapanga na kupora mali.

Akizungumza na Nipashe Kamanda wa Polisi mkoani hapo, Martine Otieno, alisema wahalifu hao wamekamatwa katika maeneo mbalimbali wakiwa na makosa tofauti.

Alisema operesheni endelevu ya kusaka wahalifu inayoendelea mkoani hapo ni kuhakikisha mji wa Dodoma unakuwa salama na wahalifu.

"Operesheni ya kusaka wahalifu inaendelea Jeshi la Polisi hatuhitaji kuona uhalifu unaenea mkoani hapo," alisema Kamanda Otieno.

Aliwataka wananchi kuendelea kutoa taarifa ndani ya jeshi hilo endapo wanaona kuna sehemu uhalifu unafanyika na watu mbalimbali.

"Tunaomba wananchi mwendelee kutoa ushirikiano mnapoona kuna uhalifu unafanyika ili Jeshi la Polisi liendelee kufanya kazi yake.

Kuhusu suala la watu wanaojiita panya road, alisema kwa upande wa Dodoma halina nafasi na kuwataka wananchi kuendelea kuwa watulivu wakati jeshi hilo likiendelea na msako wa kuwasaka wahalifu.

Nelson Ivan, mmoja wa majeruhi alisema kilitokea kikundi cha watu na kuvamia Mtaa wa Relini uliopo Kata ya Kizota na kuanza kuwasachi watu na kupora vitu vyao.

Alisema tukio hilo lililotokea juzi limezua taharuki kwa wananchi wa mtaa huo ambao wameliomba Jeshi la Polisi kuingilia kati.

"Tumekatwa mapanga na watu wasiojulikana tunaomba Jeshi la Polisi lifanyie kazi suala hilo.

Naye Siwajibu Rajabu, alisema watu walikuwa wameshika mapanga ambayo walitumia kama silaha za kuwajeruhi katika eneo hilo.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu, George Simbachawene, alipotembelea eneo linalotarajiwa kujengwa tangi la maji la lita 500,000 katika kijiji cha Ng'onje Jimbo la Kibwake Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Askofu Pentecostal aingilia kati tatizo la 'panya road'

Na Peter Mkwavila, DODOMA

MAKAMU Mkuu wa Kanisa la Pentecostal Holiness Association Mission Tanzania PHAM (T), Askofu Julias Bundala, ameitaka jamii kutoa ushirikiano kwa viongozi wa mitaa ili kukomesha vitendo vya uhalifu vinavyofanywa na makundi ya 'panya road'.

Rai hiyo ya Askofu Bundala alitoa jana jijini hapo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kutokana na kukithiri kwa matukio yanayofanywa na panya road.

Alisema ni muhimu jamii hususan wazazi na walezi kutoa ushirikiano wa kukomesha uhalifu huo kutokana na baadhi ya wanaofanya vitendo hivyo wanaishi nao kwenye familia zao.

"Makundi haya wengi wao ni vijana wenye umri mdogo, wanatoka kwenye familia za wazazi na walezi kwa maana hiyo wakitoa ushirikiano panya road watadhibitiwa na kukomeshwa na hali inakuwa shwari kwa raia wenyewe na mali zao," alisema.

Alibainisha kuwa kutokana na kukithiri kwa vitendo hivyo katika maeneo mbalimbali, hivi sasa watu wanaishi kwa mashaka makubwa ya kupoteza maisha yao na kuporwa mali zao. "Hivyo niombe kwa jamii, walezi na wazazi tushirikiane na vyombo vya dola kwa kutoa taarifa zilizo sahihi zitakazokamata makundi hayo na makundi mengine yatakayobainika kujihusisha na vitendo hivyo vya kihalifu," alisema.

Alisema msaada mkubwa utatoka kwa jamii kubaini wahalifu.

Pia aliomba viongozi wa ngazi za mitaa kuanzisha makundi ya ulinzi shirikishi wa sungasungu ili kuimarisha ulinzi kwenye maeneo mbalimbali.

Alisema jeshi hilo la sungusungu limekuwa likisaidia kuimarisha ulinzi kwenye makazi ya watu na kukomesha vitendo hivyo.

# Programu maendeleo sekta maji yazinduliwa

Na Renatha Msungu, DODOMA

SERIKALI imezindua awamu ya tatu ya programu ya maendeleo ya sekta ya maji ya miaka mitano kuanzia Julai, 2022 hadi Juni, 2026 ili kufikia maendeleo endelevu ya usimamizi wa rasilimali za maji nchini inayokadiriwa kugharimu Dola za Marekani bilioni 6.46.

Akizindua programu hiyo mwishoni mwa wiki, Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alisema utekelezaji wa programu hiyo unalenga kushughulikia kero za awamu zilizopita ili kufikia malengo ya maendeleo ya programu kupitia usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji.

Alisema serikali inatambua maji kama rasilimali muhimu katika kufikia Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano Awamu ya Tatu, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya 2020 - 2025 na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030.

Hata hivyo, alisema kwa kuzingatia mifumo ya mipango ya kitaifa na kimataifa, afua zote katika sekta ya maji zinatekelezwa ndani ya programu ya maendeleo ya sekta ya maji kwa kipindi cha mwaka 2006 hadi 2025 na inatekelezwa kwa awamu tatu.

"Utekelezaji wa awamu ya kwanza ulianza Julai 2009 na kumalizika Juni 2016, awamu ya pili ilianza Julai 2016 na kumalizika Juni 2022 na awamu ya tatu na ya mwisho imeanza kutekelezwa Julai 2022 na itakamilika 2026," alisema.

Hata hivyo, alisema baada ya kukamilika kwa programu ya maendeleo ya sekta ya maji awamu ya kwanza na awamu ya pili, wanajivunia mafanikio makubwa katika sekta hiyo ikiwa ni pamoja na maboresho katika usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji ikiwamo kuanzishwa kwa Bodi tisa za maji za Mabonde, Ithibati ya Maabara saba kati ya 17 za ubora wa maji, kuimarika kwa kiwango cha huduma ya maji vijijini hadi kufikia asilimia 72.3.

Alisema ili kuboresha kiwango cha huduma ya maji mijini hadi kufikia asilimia 86, uboreshaji wa usafi wa mazingira wa kaya zilizounganishwa na mifumo ya majitaka ya umma katika vituo vya kikanda hadi kufikia asilimia 13 na uboreshaji wa huduma za usafi wa mazingira kwa kaya za vijijini hadi kufikia asilimia 36.

Waziri Aweso aliziomba asasi za kiraia na wadau wote wa sekta ya maji kuendelea kusaidia sekta ya maji ambayo ni muhimu katika kuendeleza na kuendesha uchumi wa kijamii nchini.

Awali, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga, alisema pamoja na mambo mengine programu hiyo inalenga kufikia asilimia 85 vijijini na asilimia 95 mijini ya wananchi wanaopata huduma ya majisafi na salama ifikapo 2025.





## TIC yawahakikishia leseni wachimbaji

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WACHIMBAJI wadogo wa madini kutoka mikoa ya Nyanda za Juu Kusini wamehakikishiwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), kupewa leseni kubwa za uchimbaji kwa wakati endapo wataongeza nguvu ya mitaji.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Meneja wa TIC, Kanda, Venance Mashiba, alipozungumza na Nipashe kuhusu mikakati inayofanywa na kituo hicho kuwawezesha wachimbaji wadogo ili kunufaika na fursa zilizoko kwenye kituo hicho.

Alisema TIC inaendelea kuwahamasisha wachimbaji wadogo kutafuta mitaji mikubwa ili kupata sifa ya kusajiliwa kuwa wafanyabiashara wakubwa kama sharti ya kituo hicho ili kunufaika na fursa mbalimbali ikiwamo punguzo la gharama za uagizwaji wa vifaa vinavyohitajika kwenye shughuli za uchimbaji wa madini.

"Mchimbaji mdogo wa madini hawezi kunufaika moja kwa moja na fursa zilizoko ndani ya TIC hadi hapo atapokuza biashara yake na kuwa mchimbaji mkubwa, yapo mambo mengi ambayo tunayasimamia kwa mchimbaji mkubwa kama vile kusimamia shughuli zake za vibali na usajili ndani ya muda mfupi pamoja na kupata punguzo la asilimia kwenye vifaa atavyoagiza nje ya nchi," alisema Mashiba.

Alisisitiza kuwa TIC bado inaendelea kuwahamasisha wachimbaji wadogo kujiunga kwenye kituo hicho ili kunufaika na fursa mbalimbali zilizoko kwenye sekta ya madini kama vile masoko na unafuu wa uendeshaji shughuli hizo.

Baadhi ya wadau wa sekta ya madini wamesema wachimbaji wadogo bado wanafanya kazi kwenye mazingira magumu ikiwamo tozo kutoka mashirika na taasisi mbalimbali na kusababisha wasipate faida kwenye shughuli zao.

Amos Abraham, mchimbaji mdogo wa madini wilayani Chunya, alisema endapo serikali itaondoa baadhi ya tozo itawasaidia kupata faida kuliko ilivyo sasa na faida yote inaishia kwenye kulipa gharama hizo.

Alisema, kilio kingine kwa wachimbaji hao ni serikali kuwajengea kituo kitakachokuwa na jukumu ya kuwasaidia wachimbaji hao kupimiwa maeneo yote yenye madini.

Alisema kufanya hivyo itasaidia kurahisisha shughuli za upatikanaji na uchimbaji wa madini na kuokoa uharibifu wa mazingira unaojitokeza wakati wa kutafuta madini ya dhahabu wilayani humo.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Benjamin Kuzaga, akitoa ufafafuzi kwa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, namna magari yatakavyopita kwenye barabara ya mchepuko ya Inyala ambayo imejengwa kwa lengo la kupunguza ajali za mara kwa mara mwishoni mwa wiki. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Sampuli kuchunguzwa sumu iliyotumika mwalimu kujiua

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani hapo kwa kushirikiana na wataalamu wa afya, wamechukua sampuli kwenye mwili wa aliyekuwa mwalimu wa shule ya msingi ya mchepuo wa Kiingereza Mbuje, Saimon Mtambo kwa uchunguzi kubaini kitu alichokitumia hadi kukatisha uhai wake baada ya kutekeleza mauaji ya mke na watoto wake, hivi karibuni.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Benjamin Kuzaga, alisema hatua hiyo inalenga kubaini kitu alichokitumia mwalimu Mtambo kukatisha uhai wake kutokana na mazingira ya kifo yalivyotokea.

Alisema sampuli kwenye mwili wa Mtambo ilichukuliwa kabla ya kufanya maziko ya mke wake, Fortunata Abraham (36), aliyekuwa mwalimu wa Shule ya Msingi Ikuti, jijini Mbeya na watoto wake wawili.

"Licha ya miili ya marehemu hao wanne kukutwa imeharibika ndani ya nyumba yao eneo la Kibumbe, Kata ya Kiwira, wilayani Rungwe, mazingira ya vifo hivyo yalionesha mke na watoto walipigwa na vitu butu kwa sababu tulikuta nyundo na mapanga pembeni ya miili hiyo huku kukiwa na majeraha vichwani," alisema Kamanda Kuzaga.

"Vilevile, tulikuta kijiko na kitu kinachodhaniwa kuwa ni sumu pembeni ya mwili wa mwalimu Mtambo hivyo katika kuthibitisha hilo tumechukua sampuli kubaini ukweli."

Kuzaga alisema huenda sababu ya mauaji hayo ni mgogoro wa ndoa kutokana na kaka wa marehemu Fortunata kudai kuwa mara kwa mara walipata malalamiko kuhusu ndoa hiyo.

Kutokana na hali hiyo alisema uamuzi aliouchukua Mtambo kukatisha uhai wa mke na watoto ni unyama kwa kuwa licha ya kuwapo kwa mgogoro wa ndoa yao, angetumikia busara kushughulikia suala hilo kuliko kukatisha uhai wa watoto wake ambao hawakuwa na hatia.

Aliishauri jamii hususani wana ndoa wanapopitia nyakati ngumu kwenye familia zao kutumia wataalamu wa saikolojia ambao watawasaidia namna ya kukabiliana na mambo wanayoyapitia na kutumia madawati ya kijinsia.

Diwani wa Kata ya Kiwira, Michael Mwamwimbe, alisema huenda mauaji hayo yalitekelezwa wiki tatu zilizopita kutokana na watu hao kutoonekana kwa kipindi kirefu.

Aidha, alisema chanzo kikubwa cha mauaji hayo ni mgogoro wa ndoa wa muda mrefu uliokuwa ukisuluhishwa mara kwa mara kutokana na tuhuma zilizokuwapo kuhusu usaliti ndani ya ndoa hiyo.

Aliwashauri wanandoa wengine endapo kumetokea mgogoro kwenye familia kuhusu ndoa ni bora ikavunjwa kuliko kuendelea kuvumilia na matokeo yake ni kufikia hatua ya kutoana uhai.

"Ipo haja baadhi ya mitazamo katika jamii kwamba wana ndoa hawapaswi kutengana au kuachana na endapo ikitokea jamii itawachukulia tofauti ikapuuzwa ili kuokoa maisha ya watu na kulinda furaha zao kuliko kuvumilia mateso, majeraha na kutoana uhai," alisema Mwamwimbe.

Aliwataka wanandoa kuwa huru endapo kuna vikwazo kwenye ndoa zao ambavyo ni usaliti na masuala mengine ambayo yanakosesha amani kuachana na kila mmoja kuendelea na maisha yake kuliko kuendelea kuvumilia au kung'ang'ania ndoa ambayo tayari imeingia doa.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vicent Anney, alisema tayari miili hiyo ilizikwa wilayani humo na akatoa rai kwa wananchi kuacha kujichukulia sheria mkononi ya kujeruhi au kuua watu kutokana na migogoro ya aina mbalimbali.

Alisema kila mwananchi anapaswa kuheshimu na kulinda haki ya kuishi kwa mwenzake na kwamba endapo kuna tatizo ni busara likiripotiwa kwenye vyombo vya sheria kama vile polisi au mahakamani ili hatua zaidi zichukuliwe.

# Kaya 8,000 Mpandapanda zanufaika mradi wa majisafi

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

ZAIDI ya kaya 8,000 zilizoko kwenye kijiji cha Mpandapanda, Kata ya Kiwira, wilayani Rungwe, zimeanza kunufaika na mradi wa maji wenye thamani ya Sh. milioni 535 ambao unazalisha lita 19,000 kwa siku.

Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa mwaka huu, Sahili Nyazabara, akizindua mradi huo, alisema mradi huo unatokana na fedha za UVIKO-19 ambazo serikali ilitoa kwa ajili ya kukamilisha miradi mbalimbali ya maendeleo.

Alisema mradi huo umetekelezwa na Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA), ambao wamewasaidia wananchi kupata uhakika wa maji kwenye eneo lao ukilinganisha na ilivyokuwa awali, licha ya wilaya hiyo kubarikiwa vyanzo vingi vya maji, lakini hakukuwa na miundombinu rafiki ya kuweza kupata majisafi na salama ya bomba.

Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, alisema vituo 16 vitasaidia kusambaza huduma ya maji kwenye vijiji vyote vilivyopo kwenye Kata ya Kiwira.

"Nawasihi wateja wetu ambao mtapata huduma hii ya maji kuwa wepesi kulipia ankara zenu za matumizi ya maji kwa sababu kuna malalamiko kutoka kwa watendaji wa hizi mamlaka za maji kwamba hamlipi kwa wakati bili hali inayosababisha baadhi ya huduma zisiboreshwe na kuanza kulalamika tena," alisema Mhandisi Mahundi.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vicent Anney, alisema kukamilika kwa mradi huo kutasaidia wananchi kupata kwa ukaribu huduma za majisafi na salama ya bomba na kuchochea shughuli za kiuchumi kama vile kilimo cha mboga. Tupelike Alinanuswe alisema kukamilika kwa mradi huo kutawezesha mamalishe kufanya shughuli zao kwa urahisi.

Alisema ana uhakika kwamba biashara yake itamletea manufaa kwa kuwa muda mwingi atautumia kuwahudumia wateja wake na kupata fedha nyingi zitakazomsaidia kuboresha biashara yake na kutumiza malengo aliyojiwekea.





# 'Sekta binafsi ina mchango kudhibiti biashara haramu'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MENEJA wa Sekta Binafsi kutoka Mradi wa Tuhifadhi Maliasili, unaoendeshwa na Shirika la Msaada wa Marekani (USAID), Elikana Kalumanga Ngallaba, amesema sekta binafsi ina mchango mkubwa kudhibiti biashara haramu ya rasilimali za maliasili.

Aliyasema hayo jana Mjini Zanzibar wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya mkutano wa majadiliano kati ya sekta binafsi na serikali kuhusu uhifadhi wa rasilimali ulioandaliwa na taasisi ya sekta binafsi Tanzania.

Alisema sekta binafsi ushiriki wake haukuwa wa wazi katika uhifadhi wa maliasili hivyo wameamua kuongeza ushiriki wa sekta hiyo katika usimamizi wa rasilimali za wanyamapori, msitu na viumbe vya baharini.

Alisema lazima kuzijengea uwezo taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali katika usimamizi wa rasilimali Tanzania na kuzuia uharibifu ikiwamo biashara haramu ya wanyamapori, misitu na rasilimali za bahari.

Alisema mkutano huo unaangazia sera na sheria za nchi kwa namna gani zinatumika kuhifadhi rasilimali na inapohitajika uboreshaji wa sera na sheria kuhakikisha usimamizi wake unaenda vizuri.

Ngallaba alisema kitu chenye athari kubwa katika usimamizi wa rasilimali ni biashara haramu ya wanyamapori, misitu na viumbe vya baharini.

Alisema wameanza kutoa elimu kwa wadau ikiwamo taasisi zinazosafirisha abiria na mizigo viwanja vya ndege kufahamu biashara haramu ya wanyamapori, misitu na viumbe vya baharini na wadau hao wana mchango katika kuzuia biashara hiyo.

Alisema madhara ya biashara haramu yapo kiuchumi mfano utalii ambao zaidi ya asilimia 80 una hitaji viumbe vya baharini, misitu na wanyamapori, uharibifu wa mazingira ya bahari ikiwamo matumbawe ambayo ni mazalia ya samaki.

"Baada ya mafunzo haya tunategemea kuongezeka kwa mchango wa sekta binafsi katika kuchangia juhudi za serikali katika kupambana na biashara haramu ili kizazi kijacho kifaidike," alisema.

Aidha, alisema biashara haramu zinazosafirishwa kwa wingi ni kasa kwa mazao ya baharini ambayo ina madhara makubwa na viumbe hivyo vipo katika hatari ya kutoweka hasa ikizingatiwa kuwa viumbe hivyo vinachangia kukuza sekta ya utalii.

Alisema kwa upande wa misitu kuna milima ambayo ina viumbe wengi na baadhi vinapatikana katika misitu ya hifadhi Tanzania pekee ikiwamo vinyonga.

Alisema kuna ongezeko kubwa la usafirishaji wa viumbe hao, ikiwamo faru na meno ya tembo na wanauawa na kwa sasa wapo katika hatari ya kutoweka.

"Tuna viumbe wengi sana ambao tayari wameshatoweka kulikochangiwa na biashara haramu ya usafirishaji wa viumbe hivyo," alisema.

Hata hivyo, alisema athari nyingine ni mabadiliko ya tabianchi ambayo yamekwamisha shughuli za kilimo na watu kujiingiza katika biashara hizo haramu ili kujipatia kipato.

Alisema mabadiliko hayo yamewafanya viumbe ambao waliokuwa wakijificha kwenda katika sehemu zenye harakati za watu na kuuliwa, mahitaji mbalimbali ambayo viumbe hao wanayahitaji ikiwamo maji au malisho.

Naye mratibu wa mradi kutoka sekta binafsi Tanzania, Max Rugaimukamu, alisema sekta binafsi zina umuhimu wa kuendelea kuzilinda rasilimali ili kukuza utalii na nchi kupata pato la taifa.

"Tunatarajia matukio makubwa baada ya mafunzo haya ikiwamo kuzuia usafirishaji haramu wa wanyamapori," alisema.

Alisema vivutio vilivyopo Tanzania ikiwamo wanyamapori, viumbe vya bahari vikitoweka utalii utakufa kwa sababu Tanzania inategemea sekta ya utalii katika kukuza uchumi wake.

Washiriki wa mkutano huo, walisema elimu waliyopatiwa ni nzuri kwa kazi zao hasa ikizingatiwa kuwa viwanja vya ndege vinatumiwa na watu mbalimbali na watajua uhalali wa usafirishaji wa rasilimali ikiwamo viumbe hai.



Mwenyekiti wa Nuru Foundation, Zainab Kombo Shaib ambaye ni mke wa Makamu wa Kwanza wa Rais akimbeba mtoto Huldat Faki mwenye tatizo la kichwa kikubwa na mgongo wazi alipowatembelea katika nyumba yao ya matumaini iliyoko Mwanakwerekwe, Wilaya ya Magharibi B Unguja. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wadau uchumi wa buluu watakiwa kujadili mafanikio

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Suleimana Masoud Makame, amesema wadau wa uchumi wa buluu wana wajibu mkubwa wa kujadili rasimu ya uchumi huo pamoja na mafanikio yake.

Aliwataka wadau hao wanaopitia rasimu hiyo kuangalia maeneo muhimu ambayo yataonyesha matumizi bora ya bahari ili kuvutia wawekezaji na kubadilisha uchumi wa nchi.

Alisema hayo jana wakati akifungua mkutano wa siku moja wa kitaaluma wa kupitia rasimu ya uchumi wa buluu uliofanyika mjini hapa.

Alisema endapo rasimu hiyo itaangalia vipaumbele muhimu vya serikali kupitia uchumi huo ikiwamo changamoto ya mabadiliko ya tabianchi, matumizi bora ya nishati mbadala pamoja na kupunguza uchafuzi wa mazingira ya bahari itasaidia kuongeza ajira kupitia rasilimali za bahari.

Pia sera ya uchumi wa buluu inakwenda kugawa maeneo ya bahari juu ya mambo muhimu ikiwamo maeneo ya uvuvi, upandaji wa mwani na mambo mengine ili kuifanya bahari kuu kuwa kitu muhimu katika kufikisha maendeleo ya uchumi huo.

Alisema kukamilika kwa rasimu hiyo kutatoa tija na ufanisi wa utekelezaji wa shughuli mbalimbali za matumizi ya rasilimali ya bahari kupitia taasisi za serikali na binafsi.

Aidha, alisema licha kujadiliwa kwa rasimu ya uchumi huo, bado kuna umuhimu mkubwa wa kuitunza bahari ili kuiweka salama katika hali ya uchafuzi wa mazingira na lengo la uchumi wa buluu kukamilika. Kadhalika, alisema Shirika la Maendeleo la UNDP, limeanza kuona umuhimu wa kuwapo kwa sera hiyo na ndiyo maana wakawakutanisha wadau mbalimbali kutoka Zanzibar na Tanzania Bara lengo likiwa ni kujadili na kufikia mapendekezo yake.

Naye Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Aboud Suleiman Jumbe, alisema sera ya uchumi wa buluu chimbuko lake ni Zanzibar na ndiyo maana mkutano huo umefanyika mjini hapo kuonesha uhalisia wa jambo hilo.

Alisema wizara yake imejipanga kuwa na sera hiyo inajadiliwa na kuwa bora zaidi kwa maendeleo ya Zanzibar na Tanzania na wana imani kuwa ikiwa bora maendeleo makubwa ya uchumi wa buluu yatafikiwa.

Kwa upande wake Kaimu Mwakilishi wa Umoja wa Mataifa (UN), Ofisi ndogo ya Zanzibar, Ambrose Mugisha, alisema mkutano huo unalenga kuleta maendeleo katika sekta ya uchumi wa buluu Tanzania na utatoa fursa kwa wananchi wanaotumia bahari kujua namna sahihi ya matumizi ya bahari ikiwamo kulinda mazingira ya bahari ili kuepusha kuua viumbe vya baharini.

"Kupatikana kwa sera madhubuti inaenda kuleta mapinduzi makubwa katika maeneo ya bahari kulindwa na uchafunzi wa mazingira, kudhibiti kwa viumbe hai vya baharini na kufanya bahari kuwa salama wakati wote," alisema.

# TCRA yahakikisha upatikanaji mawasiliano uhakika Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIKA kuhakikisha wananchi wa Zanzibar wananufaika na fursa zinazopatikana kwenye mtandao na kukuza uchumi chini ya falsafa ya kujenga uchumi wa buluu; Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imesema kuwa upatikanaji wa mawasiliano ya uhakika kwenye visiwa hivyo utaendelea kuboreshwa ili wananchi wote wakiwamo wanaoishi kwenye visiwa vidogo washiriki kikamilifu kujenga uchumi.

Akizungumza jana wakati wa kampeni ya kuelimisha wananchi kuhusu fursa zinazopatikana kwenye mawasiliano na matumizi sahihi ya huduma hiyo "Kwea Kidijitali" iliyofanyika viwanja vya Mapinduzi Square, Kisonge, Meneja wa TCRA Ofisi ya Zanzibar, Esuvatie Masinga, alisema mamlaka hiyo imejizatiti upatikanaji wa huduma za uhakika visiwani humo ili wananchi washiriki kujenga uchumi wa buluu kupitia rasilimali zinazopatikana baharini.

"Ili wananchi wetu washiriki kujenga uchumi wao binafsi, TCRA tunasisitiza matumizi sahihi ya huduma za mtandao kwa kuwa kwenye anga la kimtandao kuna fursa nyingi sana; nasi tumejizatiti kuhakikisha Zanzibar inapata huduma zenye uhakika ili tujenge uchumi wa buluu pamoja," alisema. Meneja huyo aliwataka wananchi kuhakiki usajili wa namba zao za simu zilizosajiliwa kwa kutumia *106# ili kujua uhalali wa usajili wa laini zao za simu.

"Kukomesha utapeli kwa njia ya simu, ukipokea ujumbe wa kitapeli hasa ule 'ile pesa tuma kwenye namba hii...' tuma namba ya mshukiwa wa utapeli huo kwenda namba 15040 na moja kwa moja hatua zitachukuliwa," alisema.

Aidha, alisema TCRA kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi wanatoa elimu kwa umma kwa kuwafikia wananchi kwenye maeneo yenye mkusanyiko hasa masoko ya wazi na hadi sasa wamefika katika mikoa ya Mwanza, Mbeya, Njombe, Zanzibar, Kilimanjaro na kampeni hiyo inaendelea kuhakikisha wananchi wanatumia fursa za mtandaoni, kujilinda dhidi ya utapeli na matumizi yasiyo sahihi ya mawasiliano.

Akizungumzia kuhusu vijana wenye bunifu za TEHAMA, alisema sasa wanaweza kupata rasilimali adimu za mawasiliano ikiwamo masafa, kikoa cha DOT TZ na namba fupi (short codes) bure kupitia Tume ya Sayansi na Teknolojia, lengo likiwa kutanua wigo wa vijana kushiriki katika kujenga uchumi wa kidijitali.

"Tunawatolea wito vijana wenye bunifu za TEHAMA wajitokeze, bunifu hizi ni muhimu sana katika kuisaidia jamii yetu na kukuza uchumi wa Taifa letu, mwenye bunifu asisite kujitokeza, kwa sasa rasilimali hizi ambazo awali usingezipata hadi ulipie sasa watazipata bure, muhimu COSTECH iwatambue, wasajiliwe na wapate njia hizi muhimu za kupitisha bunifu zao katika hatua ya majaribio kabla hazijaidhinishwa kutumika, wasikae nyuma," alisisitiza Masinga. Kwa upande wao wananchi waliofika katika eneo hilo, waliipongeza TCRA kwa elimu waliyoitoa ambayo itasaidia kukuza uelewa wa matumizi ya mitandao ambao baadhi ya watu wanaitumia kinyume na taratibu.

Asha Bakari, miongoni mwa wananchi hao, alisema elimu hiyo iwe endelevu kwa sababu teknolojia ya mawasiliano inaendelea kukua.

TCRA ni Taasisi ya Serikali iliyoasisiwa mwaka 2003 kwa lengo la kusimamia mawasiliano katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

# Mashirika yanayopinga ndoa utotoni yatakiwa kufika vijijini

**Na Julieth Mkireri**

MASHIRIKA yanayojihusisha na mapambano ya kupinga ndoa za utotoni yametakiwa kufika maeneo ya vijijini, ambako kuna matukio mengi ya wasichana kuozeshwa wakiwa na umri mdogo.

Wito huo umetolewa mwishoni mwa wiki mkoani Dar es Salam na wadau waliohudhuria uzinduzi wa kampeni ya kutokomeza ndoa za utotoni hapa nchini inayoendeshwa na Shirika la Kuhudumia Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF).

Mwakilishi kutoka Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), ambaye ni Mwanasheria Mkuu wa Baraza hilo, Hassana Fatiu, alisema bado kuna mila na imani hazitambui kuhusu kuozesha watoto.

"Hata ukitunga sheria namna gani kama hujawabadilisha watu kupitia elimu hawawezi kuelewa, nendeni vijijini mkawaelimishe na kutokomeze ndoa za utotoni," alisema Fatiu.

Sophia Mbeyela, alisema watu wenye ulemavu ni kati ya waathirika wa ndoa za utotoni na wengi wao wanaozeshwa wakiwa ndani bila kujua hatua za kuchukua.

Aliomba wataalamu wa lugha za alama wafikishiwe elimu ya kupinga ndoa za utotoni ili wakawafikie wenye ulemavu wa kusikia nao waweze kuziepuka.

Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa (UN) Tanzania, Zlatan Milisic, alisema UN Tanzania inasaidiana na serikali kutokomeza ndoa za utotoni.

Alisema ni lazima jamii ishiriki kukemea ndoa hizo kwa kuwa zinaathiri kuyumba kiuchumi na kudumu katika umasikini, vifo vya watoto wachanga na wa kike wanapojifungua, pia inaongeza vifo vya wajawazito na kuharibika kwa mimba.

Katika kampeni hiyo iliyopewa jina la 'binti' ambayo inalenga kuungwa mkono kwenye jamii ilielezwa kuwa msichana mmoja kati ya watatu anaolewa kabla ya kufikisha umri wa miaka 18.

Wadau waliohudhuria uzinduzi huo waliitaka serikali kufanya marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971.

Mwakilishi wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), ambaye ni Mhariri wa habari, Gazeti la Mwananchi, Lilian Timbuka, alisema kampeni hiyo inatakiwa kufika maeneo ya vijijini na mashirika yanayohusika yanatakiwa kutumia zaidi vyombo vya habari kuelimisha jamii.



Mkurugenzi wa Hazina wa Tanzania Commercial Bank (TCB), Wenceslaus Fungamtama (kushoto), akikabidhi msaada wa viti vitano vya mbao pamoja na kompyuta kwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani (RPC), Pius Lutumo, kwa ajili ya kulisaidia Jeshi la Polisi kukabiliana na kudhibiti uhalifu wa makosa ya kimtandao. Wengine ni maofisa wa polisi kutoka Kituo cha Polisi Kibaha mkoani humo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Daraja Wami kutumika wiki ijayo

**Na Beatrice Shayo,** PWANI

KATIBU wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka, amesema serikali imeridhishwa na ujenzi wa daraja la Wami mkoani Pwani na magari yataanza kupita mwishoni mwa Septemba, mwaka huu.

Shaka aliyasema hayo jana alipotembelea mradi wa ujenzi wa daraja hilo linalogharimu Sh. bilioni 75.13 na barabara unganishi.

"Pongezi zetu ziwafikie makandarasi ndani ya kipindi kifupi tuliambiwa daraja hili lingeanza kazi Septemba 20, tukasema haitawezekana lianze kazi kabla ya chama kufika hili jambo ni kubwa," alisema.

Shaka alisema daraja hilo limebeba maslahi ya Watanzania kutokana na kuunganisha mikoa yote ya Kaskazini na nchi jirani ya Kenya.

Alisema watakwenda kufungua uchumi wa ukanda huo kutoka mikoa ya Kaskazini mpaka Mkoa wa Dar es Salaam na fursa ambazo zitatokana na daraja hilo ni nyingi hasa kiuchumi.

"Sekta ya usafiri na usafirishaji itaimarika kuliko ilivyo sasa kipindi cha nyuma madereva walikuwa wakikatisha ruti zao wakihofia usalama wa barabara hii usalama wa mali zao na wa watu wao ambao wamekuwa wakiwatuma kazi," alisema Shaka.

Alisema kukamilika kwa daraja hilo kunatoa uhakika wa maisha ya wanadamu na wanyama waliokuwa katika eneo hilo.

Vile vile, athari iliyopatikana kutokana na ufinyu wa daraja la awali ni mkubwa na Rais Samia Suluhu Hassan alipoingia madarakani kulikuwa na maneno kuhusu daraja hilo na miradi ya mikakati kutokuendelea.

# Wenye ualbino wapewa mbinu kuinuka kiuchumi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

OFISA Ustawi wa Jamii Jiji la Dodoma, Mboni Msantu, amewataka watu wenye ualbino kutumia fedha wanazosaidiwa kutoka mashirika na taasisi zisizo za kiserikali, kuanzisha miradi ili kuinuka kiuchumi.

Mboni alitoa rai hiyo jana alipozungumza na watu wenye ualbino kutoka Jiji la Dodoma na Chamwino wanaofadhiliwa na Shirika lisilo la Kiserikali la Maendeleo na Msaada la Waadventista Wasabato (ADRA) na mradi wa ujasiriamali na ajira kwa watu wenye ualbino (SEEPA).

Kundi hilo limesaidiwa zaidi ya Sh. milioni 10 kwa ajili ya kuanzisha miradi ya ujasiriamali.


Alisema fedha hizo hazina riba na wamesaidiwa na wafadhili hao kwa malengo ya kuwaondolea ugumu wa kimaisha waliokuwa nao, hivyo ni muhimu wakabuni miradi yenye tija.

"Shirika la ADRA na mradi wa SEEPA kwa pamoja wametoa fedha kwa kwenu ninyi watu wenye ualbino kutoka Chamwino na Jiji la Dodoma, tumieni fursa hiyo kwa kuzitumia kwa kuanzisha miradi itakayowaondolea hali ngumu ya kiuchumi," alishauri.

Meneja wa Mradi Mikoa ya Dodoma na Morogoro wa Shirika la Maendeleo na Misaada la Waadvestista Wasabato, Denis Robert, aliseme fedha zilizotolewa kwa watu wenye ualbino ni kwa wale wanaomba kupitia andiko ili wasaidiwe fedha kutoka kwao.

Alisema shirika hilo limekuwa likisaidia kundi hilo kwa kuwapatia elimu ya ujasiriamali ili iwabadilishe kimaisha. Mwenyekiti wa Chama cha Watu Wenye Ualbino Mkoa wa Dodoma, Ludovick Kowo aliwataka waliokabidhiwa fedha na shirika hilo, kutoziingiza kwenye bajeti ya matumizi ya anasa kwa kuwa fedha hizo kutumika kufanyia starehe ni kinyume cha maelekezo yaliyokusudiwa.

Alisema fedha hizo zilenge katika kuibua miradi kutokana na mafunzo waliyopewa ya ujasiriamali ili wabadilike na kuinuka kimaisha.



## Biden amwonya Putin matumizi ya silaha za nyuklia

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Joe Biden, ameionya Russia isitumie silaha za kemikali au silaha za kimkakati za nyuklia katika vita nchini Ukraine.

Akizungumza wakati wa mahojiano na CBC News, Biden alisema hatua ya aina hiyo itabadilisha sura ya vita iliyokuwapo kati ya nchi hizo, tofauti na kitu chochote kile tangu vita ya pili ya dunia, japokuwa hakusema ni vipi Marekani itajibu iwapo silaha za aina hiyo zitatumika.

Inaelezwa kuwa Rais wa Russia Vladimir Putin aliviweka vikosi vya nyuklia vya nchi yake katika hali ya tahadhari kutokana na uvamizi wake nchini Ukraine mwezi Februari, huku ikidaiwa kwamba aliwaambia wakuu wa ulinzi ni kwasababu ya kauli za uchokozi za Magharibi.

Aidha, kwa mujibu wa vyanzo vya kuaminika, silaha za nyuklia zimekuwapo kwa karibu miaka 80 na nchi nyingi tunaziona kama njia inayotoa hakikisho kwa usalama wa taifa husika.

Russia inakadiriwa kuwa na vilipuzi vya nyuklia takriban 5,977, kulingana na Shirikisho la wanasayansi wa Marekani, ikielezwa kuwa huwenda isiwe na uwezekano wa kutumia silaha hizo.

Pia ilibainishwa kuwa silaha za mbinu za nyuklia ni zile zinazoweza kutumiwa katika masafa mafupi, tofauti na za kimkakati za nyuklia ambazo zinaweza kupiga katika masafa marefu na kusababisha vita kamili vya nyuklia.

Katika mahojiano aliyofanyiwa na Shirika la Habari la (CBS) katika Ikulu ya White House, Rais Biden aliulizwa ni nini angemwambia Putin iwapo anaangalia uwezekano wa kutumia silaha za maangamizi nchini Ukraine, ambapo alijibu kwa msisitizo kwamba suala hilo lisifanyike.

Biden aliulizwa pia ni athari zipi zitakuwa kwa Putin iwapo mstari huo utavukwa ambapo alijibu kwamba, "Unafikiri nitakwambia iwapo ninajua ni nini? Bilas sitakuambia. Itakuwa na athari," alijibu. **BBC**

# Malkia Elizabeth II kuzikwa leo

**LONDON,** Uingereza

MWILI wa Malkia Elizabeth II unatarajiwa kuzikwa leo Westminster Abbey jijini London, ambapo Rais Samia Suluhu Hassan na Rais wa Marekani Joe Biden ni miongoni mwa viongozi watakaoshiriki katika mazishi hayo.

Inaelezwa kuwa zaidi ya viongozi 500 wa kigeni wako jijini London kwa ajili ya kushiriki katika mazishi hayo ya kitaifa, yanayowakutanisha viongozi wa ulimwengu wengi zaidi kuonekana kwa pamoja kwa miongo kadhaa.

**naelezwa kuwa zaidi ya viongozi 500 wa kigeni wako jijini London kwa ajili ya kushiriki katika mazishi hayo ya kitaifa.**

Kwa mujibu wa BBC, mawaziri wakuu wa Canada, Australia na New Zealand tayari wako Uingereza, na kwamba viongozi wengine wa Jumuiya ya Madola wanaotarajiwa kuhudhuria ni pamoja na Waziri Mkuu wa Bangladesh Sheikh Hasina na Rais wa Sri Lanka Ranil Wickremesinghe.

Ilielezwa kuwa India itawakilishwa na Rais Droupadi Murmu, na kwamba viongozi walioalikwa jana watapata nafasi ya kutoa heshima zao za mwisho huko Westminster na kutia saini kitabu cha maombolezo.

Malkia Elizabeth II, aliyehudumu



muda mrefu zaidi nchini Uingereza, alifariki Balmoral akiwa na umri wa miaka 96, baada ya kutawala kwa miaka 70. **BBC**



Mwili wa Malkia Elizabeth II ukiagwa kwa mara ya mwisho. **PICHA: MTANDAO**

# Tanzania, Uganda yaikana EU mradi bomba mafuta

SERIKALI nchini Tanzania imesema kwamba miradi yote mikubwa inayotekelezwa nchini humo inafuata sheria na kanuni za kimataifa ikiwamo za utunzaji wa mazingira na kuheshimu haki za binadamu huku ikifanya miradi yake kwa manufaa ya wananchi wake.

Hatua hiyo ilikuja baada ya Bunge la Umoja wa Ulaya (EU) kusema kwamba Tanzania na Uganda zinapaswa kusitisha mradi wake wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki lenye urefu wa kilomita 1,443 kutoka Ziwa Albert, Uganda hadi Bandari ya Tanga nchini Tanzania.

Waziri wa Nishati, Januari Makamba aliieleza BBC kuwa Tanzania inazingatia vigezo vya kimataifa katika miradi yake ikiwamo ule wa bomba la mafuta kutoka Uganda mpaka Tanga nchini Tanzania na kwamba hakuna kinachokiukwa kama azimio la bunge hilo linavyoeleza.

"Nimefuatilia mapendekezo na azimio la Bunge la Umoja wa Ulaya kuhusu ukiukwaji wa haki za binadamu na uharibifu wa mazingira, ninaona washauri juu ya mradi na athari zake, serikali ya Tanzania imefuata taratibu zote za kuhakikisha haki za watu na mazingira zinalindwa lakini hakuna kilichokiukwa.

"Tumelipa fidia wananchi wote ambao maeneo yao yapo kwenye eneo la mradi, hakuna yeyote aliyelazimishwa au kukamatwa kwa nguvu, lakini tumefuata kanuni zote zinazohusu mazingira ili mradi huu usidhuru mazingira," alisema.

Aliongeza kuwa Tanzania ina kila haki ya kuhakikisha wananchi wake wananufaika na rasilimali zilizoko kama ilivyo kwa nchi zilizoendelea ambazo wananchi wake wananufaika na miradi hiyo.

Rais wa Uganda, Yoweri Museveni, alisema nchi hiyo itamtafuta mwekezaji mwingine wa kufanya naye kazi iwapo kampuni ya mafuta ya Total Energies itachagua kusikiliza Bunge la Umoja wa Ulaya linalozitaka Uganda na Tanzania kusitisha maendeleo ya mradi wa bomba la mafuta na gesi katika nchi hizo mbili za Afrika Mashariki.

Museveni aliuambia mkutano mjini Kampala mwisho wa wiki iliyopita kuwa mradi wa mafuta utaendelea kama ilivyoainishwa katika mkataba na Total Energies na Kampuni ya Kitaifa ya Mafuta ya China (CNOOC), akieleza kuwa pipa la kwanza la mafuta litatoka mnamo 2025.

Bunge la Umoja wa Ulaya Alhamisi ya wiki iliyopita, lilionya kuhusu ukiukwaji wa haki za binadamu pamoja na hatari ya kijamii na kimazingira inayoletwa na mradi wa Bomba la Mafuta la Afrika Mashariki, (EACOP).

**BBC**

# NMB YATWAA UBINGWA WA SOKA NMB-BUNGE BONANZA

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KIKOSI cha timu ya soka ya NMB, kimeibuka wababe wa Tamasha la NMB-Bunge Bonanza 2022 'Kivumbi na Jasho,' baada ya kuichapa timu ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 'Bunge FC' kwa mabao 2-0 katika fainali ya bonanza hilo iliyopigwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Kilimani jijini Dodoma.

**NMB-Bunge Bonanza ni tamasha la siku moja la michezo baina ya timu za Benki ya NMB na Bunge, lililoanza kwa matembezi yaliyoongozwa na Spika Dk. Tulia Ackson na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB (iliyoandaa bonanza hilo), Ruth Zaipuna, kabla ya timu za kila upande kuchuana katika michezo mbalimbali.**

Baada ya Bunge SC kufanya vema katika michezo ya Kuvuta Kamba, Kukimbiza Kuku, Mpira wa Wavu, Netiboli na Kikapu kwenye viwanja vya Chinangali Park, NMB ilikuja juu na kupindua meza ya matokeo hayo kwa kushinda fainali ya soka kwa mabao ya Alex Joseph na Laurent Kilumanga.

Ukiondoa ushindi huo, NMB-Bunge Bonanza limefanyika kwa mafanikio makubwa, huku kila upande miongoni mwa timu shiriki, ukilitumia tamasha hilo kufanya mazoezi ya ushiriki wa matukio tofauti ya kimichezo, yanayohusisha timu za NMB na Bunge SC.

Wakati Bunge SC, ikilitumia bonanza hilo kunoa makucha kuelekea Mashindano ya tisa ya Mabunge ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EALA 2022), timu za NMB wamelitumia kupasha misuli moto, kujiandaa na Mbio za Hisani za NMB Marathon 2022 'Mwendo wa Upendo.'

Akizungumza wakati wa bonanza hilo, Spika Dk. Tulia, alisema wanaamini NMB-Bunge Bonanza 2022 litakuwa na mchango chanya kwa timu zao, kuelekea EALA 2022 na kwamba walipanga kulipa uzito mkubwa ili kuhakikisha linanufaisha timu zao, kama ilivyokuwa mwaka jana.

"Mwaka jana tulishiriki Mashindano ya Mabunge na tuliongoza kwa ujumla, mafanikio hayo yalitokana na ubora na uimara wa timu zetu, ambao ulianzia katika NMB-Bunge Bonanza, na tunaamini limetupa mazoezi ya kutosha mwaka huu, kutuwezesha kufanya makubwa zaidi ya msimu uliopita," alisema Spika Tulia.

Kwa upande wa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Zaipuna alisema timu zake zimeshiriki bonanza hilo kama sehemu ya uenyeji wao wa Mbio za NMB Marathon, zitakazofanyika hivi karibuni, Mgeni Rasmi akitarajiwa kuwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, zikilenga kukusanya Sh. milioni 600 za kusaidia matibabu ya kinamama wenye fistula.

"Siku chache zijazo tutakuwa wenyeji wa NMB Marathon, ndio maana tunalitumia bonanza hili kufanya mazoezi, huku tukiwaomba spika na wabunge wote, mjitokeze kujisajili ili kushiriki mbio hizo, zenye lengo la kukusanya pesa za kutibia kinamama wenye fistula katika Hospitali ya CCBRT," alisema.

Licha ya NMB kuibuka na ushindi huo katika soka, pia ilishinda mchezo wa kufukuza kuku wanaume, huku timu za Bunge zikitawala michezo mingine yote.

Katika kikapu wanaume, Bunge iliibuka na ushindi wa pointi 44-40, huku upande wa wanawake Bunge nao wakishinda baada ya NMB kutoingiza timu uwanjani.

Michezo Mingine ambayo Bunge iliishinda NMB ni Kuvuta Kamba (wanawake na wanaume), netiboli 29-4, wavu wanawake na kufukuza kuku kwa wanawake.




Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akikabidhi kombe kwa timu ya mpira wa miguu ya NMB baada ya kuifunga timu ya Bunge Sports Club mabao 2-0 katika wa mchezo uliochezwa Uwanja wa Kilimani jijini Dodoma juzi kwenye Bonanza la NMB Kivumbi na Jasho. Kushoto ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna. **MPIGAPICHA WETU**

# *Geita Gold: Tumejifunza kimataifa*

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kutolewa kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika kwa bao la ugenini, timu ya Geita Gold imesema imepambana kiasi cha kutosha na haikutolewa kinyonge, huku ikjifunza vitu vingi kwenye michuano hiyo.

Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Mathias Wandiba, alisema makosa waliyoyafanya ya kuruhusu bao ugenini na pia kuruhusu lingine nchini ndiyo yaliyowagharimu, lakini akiwapongeza wachezaji wao kwa kupambana hadi mwisho, ikitoa upinzani mkubwa kwa Hilal Alsahil SC ya Sudan.

Pamoja na ushindi wa mabao 2-1 kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi, yakifungwa na Daniel Lyanga na Edmund John, haukuweza kuwavusha kwenye raundi ya kwanza ya michuano hiyo, kwani wiki moja iliyopita ikiwa nchini Sudan ilipoteza kwa bao 1-0, hivyo matokeo ya jumla kuwa mabao 2-2, hivyo Hilal Alsahil kunufaika na bao la ugenini.

"Wachezaji wangu wamecheza vizuri, wamepambana, lakini idadi ya mabao ndiyo yametuhukumu na kututoa, wachezaji wamejituma, wamefuata maelekezo, lakini kukubali kuruhusu bao kwao na hapa dakika ya nne tu ndiyo imesababisha yote haya. Mwisho wa siku nawapongeza vijana wangu, wameonyesha upinzani, basi tunakwenda kupambana kwenye Ligi Kuu na Kombe la FA," alisema Wandiba.

Alisema katika mechi zote mbili, ya juzi ilikuwa ngumu zaidi, akiongeza kuwa kipindi cha kwanza vijana wake hawakuwa na kasi, lakini cha pili waliongeza kasi na kuwaweka roho juu wapinzani wao, ila kwa bahati mbaya imeshindikana.

"Tumejifunza kuwa michuano hii ni mizito na inahitaji maandalizi makubwa kuanzia viongozi, makocha mpaka wachezaji, angalia mechi hii Sudan si nchi ndogo kwenye soka hata timu ya taifa, kwa hiyo tunarudi kusaka tena nafasi ya kuiwakilisha nchi, tutarudi tukiwa tumejifunza mambo mengi," alisema.

# Lusajo sasa awakimbiza Mayele, Phiri

**Na Cheji Bakari,** TANGA

STRAIKA wa Namungo FC, Reliants Lusajo, ameendelea kuwakimbiza mastraika wa Ligi Kuu Bara akiwamo Fiston Mayele wa Yanga na Moses Phiri wa Simba.

Lusajo juzi alifunga bao pekee wakati Namungo ikishinda 1-0 dhidi ya Coastal Union ya Tanga kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Majaliwa mkoani Lindi, hivyo mshambuliaji huyo kufikisha mabao matano, moja mbele ya Mayele mawili mbele ya Phiri wakati huu ligi hiyo ikiwa raundi ya nne.

Katika michezo minne iliyocheza, Namungo FC imeshinda michezo mitatu na kutoa sare mchezo mmoja, hivyo kufikisha pointi 10 sawa na Yanga iliyopo kileleni mwa ligi hiyo na Simba inayoshika nafasi ya pili, zote zikizidiana kwa tofauti ya mabao tu.

Mabao ya Lusajo, ndiyo yaliyotoa mchango mkubwa katika kuifikisha Namungo katika nafasi hiyo ya tatu ikiwa na alama sawa na vigogo hao wa soka nchini.

Lusajo alianza kutupia katika mchezo wa kwanza wa Ligi Kuu Bara Agosti 15, mwaka huu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam dhidi ya Mtibwa Sugar wakati timu hizo zikitoka sare ya mabao 2-2 huku mshambuliaji huyo akicheka na nyavu mara mbili dakika ya 33 na 82 ya mchezo huo.


Agosti 19, mwaka huu wakati Namungo FC ikicheza dhidi ya Mbeya City Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, alirudi tena kambani kwa kuipa timu yake bao pekee wakati ikishinda 1-0.

Katika mchezo wa mzunguko wa tatu wa Ligi Kuu Bara, Lusajo alizichungulia tena nyavu na kuipa Namungo FC ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Ruvu Shooting katika Uwanja wa Majaliwa kabla ya juzi kuitungua Coastal Union.



## ZISIKUPITE

### SKRINIAR AWANIWA CITY



KLABU ya Manchester City imejiunga na Tottenham na Chelsea kumfuatilia mlinzi wa Inter Milan na Slovakia, Milan Skriniar mwenye umri wa miaka 27. ***(Sun)***

### JORGINHO AFIKIRIWA BARCA

BARCELONA wanafikiria kumsajili nyota wa Chelsea, Jorginho msimu ujao wa majira ya joto, wakati mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 raia wa Italia atakapokuwa huru. ***(Mirror)***

### WALKER ASUBIRISHWA CITY



MANCHESTER City watasubiri hadi baada ya Kombe la Dunia kufungua mazungumzo na mlinzi, Kyle Walker mwenye umri wa miaka 32, ili kuongeza mkataba mpya. ***(Star)***

### LUKAKU KUACHIWA CHELSEA

CHELSEA ipo tayari kufikiria dili la mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 29, kuhusu kuhamia moja kwa moja Inter Milan, ambako kwa sasa anacheza kwa mkopo. ***(CalcioMercato)***

### FRANK KUMRITHI RODGERS



KLABU ya Leicester City inaweza kufikiria kumchukua kocha wa Brentford, Thomas Frank kama wakiachana na Brendan Rodgers. ***(Telegraph)***

### TSYGANKOV AWINDWA

KLABU ya Newcastle United inafikiria kumsajili winga wa Dynamo Kyiv, Viktor Tsygankov katika dirisha la Januari, lakini Borussia Dortmund, RB Leipzig, Wolves na West Ham pia zinamwania mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 raia wa Ukraine. ***(Jeunes Footeaux)***

### DIABY NA LEVERKUSEN



KLABU ya Bayer Leverkusen iko tayari kumwachia winga, Moussa Diaby mwenye umri wa miaka 23, ambaye anawaniwa na Chelsea, Tottenham, Arsenal, Manchester City na Newcastle United. ***(90min)***

### GRIEZMANN AMULIKWA UTD

MANCHESTER United inaweza kuangalia uwezekano wa kumsajili fowadi wa Barcelona mwenye umri wa miaka 31, Antoine Griezmann, Januari. ***(Daily Express)***

### GOMES ATAJWA LIVERPOOL



KLABU za Liverpool na Manchester United zinamwania kumsajili kiungo wa Flamengo mwenye umri wa miaka 21, Joao Gomes katika dirisha la Januari. ***(CalcioMercato)***

### OBLACK KUMRITHI DE GEA

MANCHESTER United wanamtaka golikipa wa Slovenia na Atletico Madrid, Jan Oblak, 29, ili kuziba nafasi ya David de Gea. ***(Jeunes Footeaux via Sun)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# SON AFUNGUKA MAZITO HAT-TRICK KWA LEICESTER

**LONDON,** England

**●●● Ilikuwa utendaji wa hali ya juu, jinsi ninavyocheza, naweza kufanya vizuri zaidi kuliko...**

SON Heung-min alihisi "amewakatisha tamaa" wachezaji wenzake wa Tottenham Hotspur kabla ya kufungua akaunti ya mabao msimu huu kwa hat-trick ya kuvutia dhidi ya Leicester City, Jumamosi.

**Mchezaji huyo wa kimataifa wa Korea Kusini aliingia akitokea benchi katika kipindi cha pili cha mchezo huo wa Ligi Kuu England na kufanya vema katika mchezo ambao waliibuka na ushindi wa mabao 6-2 dhidi ya 'Mbweha' hao.**

Baada ya kubadilishwa kwenye kikosi cha kwanza na Dejan Kulusevski, uchezaji wa Son kama mbadala ulikuwa ukumbusho wa kipaji chake kwa wakati unaofaa.

Katika mechi nane zilizopita msimu huu, zikiwamo mbili za Ligi ya Mabingwa Ulaya, Son alishindwa kufunga na alitoa pasi moja pekee.

Akizungumza baada ya mchezo huo, alisema kitendo hicho kilimuacha na hisia, baada ya wiki kadhaa za kuhisi ameiangusha klabu.

"Ilikuwa utendaji wa hali ya juu," alisema Son akiiambia Sky Sports.

"Jinsi ninavyocheza, naweza kufanya vizuri zaidi kuliko nilivyofanya. Nilikata tamaa, nilitaka kufanya kila niwezalo kwa ajili ya timu. Nitajitahidi kufanya hivyo ninapocheza.

"Ninapata hisia. Kumekuwa na usaidizi wa ajabu, na mara zote nimekuwa nikijisikia kama nimewakatisha tamaa wachezaji wenzangu na mashabiki kwa uchezaji wangu. Wamekuwa wakiniunga mkono kila mara."

Mchezo huo wa Son ulimfanya kuwa mchezaji wa saba katika historia ya mashindano hayo kufunga hat-trick baada ya kuingia kama mchezaji wa akiba, na kuisaidia Tottenham kuwa kileleni mwa jedwali na Manchester City, ingawa wanatofautiana mabao.

Wakiwa na pointi 17 katika mechi saba na rekodi ya kutopoteza ya kuanza msimu huu, vijana hao wa kocha Antonio Conte wamekuwa na mwanzo wao bora wa msimu wa Ligi Kuu England.

Na Conte raia wa Italia hakika alifurahi kumuona Son akifungua ukurasa, huku akisema: "Nina furaha sana kwa Sonny leo (juzi), anajua ninachofikiria kuhusu mchezaji huyo.

"Nilimwambia, 'ikiwa utafunga mabao matatu ndani ya dakika 30, labda tunaweza kuwa bora zaidi', lakini nilikuwa natania.

"Nina bahati, nina kundi zuri la wachezaji, ambao ni watu wazuri sana. Inabidi tuanze kufikiria kwa njia tofauti ikiwa tutapiga hatua inayofuata."

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
TENERIFE
VERSUS
MALAGA
1 | 1.98
X | 3.19
2 | 3.84

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# GREALISH AMSHUKURU GUARDIOLA



**MANCHESTER,** England

JACK Jack Grealish alimshukuru Pep Guardiola baada ya kufunga bao lake la kwanza msimu huu katika ushindi wa mabao 3-0 wa Manchester City dhidi ya Wolves, akikiri wakosoaji walikuwa sahihi kuhoji uchezaji wake.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England alifungua akaunti yake kwa kampeni hiyo baada ya sekunde 55 akiwa pale kwenye dimba la Molineux alipotumia mguso wa mwisho kwa krosi ya Kevin De Bruyne.


Grealish, ambaye alitikisa nyavu mara sita katika msimu wake wa kwanza akiwa City baada ya kuhama kutoka Aston Villa kwa pauni milioni 100, alitolewa katika dakika ya 58 ya ushindi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Borussia Dortmund katikati ya wiki.

Alifurahi kuanza akifunga bao lake la kwanza tangu sare ya mabao 2-2 na West Ham Mei mwaka huu na anatumai kuendelea kulipa imani ya Guardiola.

"Ilikuwa ni muda mrefu kuja na ni nzuri kutoka kwenye alama," alisema Grealish akiiambia BT Sport.

"Ni kweli, watu wamekuwa wakiuliza maswali, natakiwa kufunga zaidi na kupata pasi nyingi za mabao.

"Siku zote nitakuwa na watu wanaozungumza juu yangu na fedha ambazo zilitumika kuninunua, lakini kazi yangu yote sijafunga mabao ya kutosha. Nataka kuongeza hilo kwenye mchezo wangu.



## 'Kila timu imejiandaa kushinda'

**BARCELONA,** Hispania

KOCHA Mkuu wa Barcelona, Xavi anaamini "kila mtu yuko tayari" wakati aliposhuhudia umuhimu wa wachezaji wa kikosi chake baada ya ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Elche iliyokuwa na wachezaji 10 uwanjani pale Camp Nou.

Bao la Memphis Depay na mabao mawili ya Robert Lewandowski yaliifanya Barca kuibuka na ushindi wa tano katika mechi sita za kwanza za LaLiga.

Pointi hizo tatu ziliwafanya kuwa kileleni mwa jedwali kabla ya mechi ya jana Jumapili ya Real Madrid na Atletico Madrid na Xavi anaamini kuwa kila timu imejiandaa vema msimu huu.

"Sisi ni kikosi kipana, ambacho kila mmoja anafanya mazoezi vizuri. Kila mtu amejiandaa na kuunganishwa wakati timu inapohitaji, na hilo ndilo muhimu," alisema Xavi.

"Ni mwaka wa kawaida na ratiba ngumu. Hatutapumzika kwa wiki chache, na tunahitaji kila mtu. Ni juu ya kuunda kikundi. Yeyote anayecheza, timu iko kwenye jukumu.

"Tuna mengi ya kuchagua na mwishowe vikosi ndivyo vinashinda mataji."

## HABARI MICHEZO

CHEZA USHINDE KASINO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

# KIPANGA KUWAVAA WATUNISIA IKILENGA KUTINGA MAKUNDI CAF

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BAADA ya kufanikiwa kutinga raundi ya Kwanza ya Kombe la Shirikisho Afrika kwa mara ya kwanza katika historia yake, timu ya Kipanga FC ya Zanzibar, imesema lengo lake ni kufika hatua ya makundi ya michuano hiyo msimu huu.

**Kipanga juzi iliitoa Al Hilal FC Wau ya Sudan Kusini kwa mikwaju ya penati 4-3 katika mchezo wa marudiano wa michuano hiyo uliopigwa Uwanja wa Amaan, Zanzibar.**

Hatua hiyo ya mikwaju ya penalti ilichukua nafasi yake baada ya mechi kumalizika kwa sare bao 1-1 kama ilivyokuwa mchezo wa kwanza wa ugenini kwa Kipanga uliopigwa Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam ambao Al Hilal FC Wau waliutumia kama dimba lao la nyumbani kikanuni kutokana na hali ya usalama nchini kwao kutokuwa shwari.

Kipanga licha ya kushiriki michuano ya kimataifa kwa miaka mingi, haijawahi kuvuka hatua ya awali, hivyo msimu huu kutinga raundi ya kwanza ni historia kubwa kwao.

Akizungumza na gazeti hili kwa furaha, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Khamis Hassan alisema ni furaha kwa kutimiza lengo lao la kwanza, hivyo watahakikisha wanasonga mbele katika michuano hiyo ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Alisema hatua ya kwanza wamemaliza na sasa wanasubiri kukutana na Club Africain ya Tunisia kati ya Oktoba 7-9, mwaka huu, ambapo wataanzia nyumbani katika Uwanja wa Amaan.

Hassan alisema malengo makubwa ya timu hiyo ni kuhakikisha inafika hatua ya makundi katika michuano hiyo ya kimataifa ili kuzipa hamasa timu nyingine za Zanzibar ziweze kufanya vizuri zinapopata nafasi ya kuiwakilisha nchi katika mashindano hayo.

Aidha, alisema kusonga mbele katika michuano hiyo imekuwa kama mshtuko kwa mashabiki wa soka Zanzibar kwani mara nyingi walizoe kuona timu zao zinazowawakilisha katika michuano ya kimataifa zikiishia hatua ya awali.

Hata hivyo, alisema kwa sasa timu hiyo inaendelea na maandalizi ya mechi za Ligi Kuu Zanzibar pamoja na mchezo huo dhidi ya Club Africain, ambayo yenyewe imeanzia moja kwa moja hatua ya Kwanza.

WETU HUU...




Mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele na kiungo Feisal Salum 'Fei Toto' katika harakati za kuwania kufunga dhidi ya wachezaji wa Zalan FC ya Sudan Kusini kwenye mchezo wa awali mkondo wa pili wa Ligi ya Mabingwa Afrika uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi. Yanga iliibuka na ushindi wa mabao 5-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Mbeya Kwanza yaanza vema Championship*

**Na Adam Fungamwango**

USHINDI wa mabao 2-1 ugenini dhidi ya Gwambina, umeifanya timu ya Mbeya Kwanza iliyoshuka daraja msimu huu kuanza vema Ligi ya Championship kwenye harakati za kutaka kurejea tena Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kwenye moja kati ya mechi za ufunguzi wa ligi hiyo iliyoanza juzi kwenye viwanja mbalimbali nchini, Mbeya Kwanza ilikuwa Uwanja wa Gwambina juzi na kuwaduwaza wageni ikipata ushindi huo, huku timu nyingine iliyoshuka daraja msimu huu Biashara United ikianza vibaya kwa kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Fountaine Gate kwenye Uwanja wa CCM Gairo, Morogoro.

Maafande wa JKT Tanzania ambao nusura wapande Ligi Kuu msimu huu kabla ya kutolewa kwenye mechi ya mchujo dhidi ya Prisons, walianza vema kampeni yao ya kutaka kurejea kwenye Ligi Kuu kama ilivyokuwa miaka kadhaa iliyopita, ilipoiangamiza Copco mabao 2-0, mechi ikichezwa Uwanja wa Meja Isamuhyo, Dar es Salaam.

Kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza, Pamba ilipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya KenGold, African Sports ikilazimishwa sare ya bao 1-1 nyumbani, Mkwakwani dhidi ya Green Warriors na Mabingwa wa Jamhuri ya Muungano mwaka 1982, Pan African, ikiwabana mbavu nyumbani Ali Hassan Mwinyi, Tabora mwenyeji Kitayosce.

Mashujaa ikiwa Lake Tanganyika, Kigoma, ililazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Transit Camp, huku Mbuni FC ya Arusha ikiisasambua Ndanda FC mabao 3-0 kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid.

Baada ya mechi za raundi ya kwanza kukamilika, Mbuni FC iko kileleni ikiwa na pointi tatu na mabao matatu, huku Mbeya Kwanza ikishika nafasi ya pili kwa pointi tatu na mabao mawili.


## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATATU - 19/09/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 1651 | KF Ferizaj vs KF Ballkani | 5.52 | 3.79 | 1.53 |
| 16:00 | 2562 | Besa vs Apolonia Fier | 2.05 | 4.40 | 2.75 |
| 16:00 | 2965 | CA River Plate (Arg) vs San Lorenzo de Almagro Res. | 1.56 | 3.89 | 4.92 |
| 16:00 | 3422 | Kukesi vs Partizani Tirana | 2.90 | 3.09 | 2.32 |
| 17:00 | 1138 | NK Bistrica vs NK Rogaska | 2.85 | 3.34 | 2.22 |
| 17:00 | 2699 | CA Aldosivi Reserve vs Arsenal FC Reserve | 2.26 | 3.09 | 2.99 |
| 17:00 | 3158 | Velez Sarsfield Reserve vs CA Tigre Reserve | 1.58 | 3.78 | 4.91 |
| 17:00 | 3643 | Atletico Tucuman Reserve vs Argentinos Juniors Reserve | 3.33 | 3.14 | 2.08 |
| 17:00 | 4626 | Velez Mostar vs FC Sarajevo | 2.14 | 3.18 | 3.13 |
| 17:00 | 5955 | Al-Yarmouk vs AL Karmel | 2.20 | 3.05 | 3.15 |
| 18:00 | 4734 | Kolubara vs Novi Pazar | 2.76 | 3.25 | 2.33 |
| 19:00 | 1688 | Urartu vs Pyunik Yerevan | 2.89 | 2.99 | 2.38 |
| 19:00 | 1722 | Ullensaker/Kisa vs Valerenga IF 2 | 1.23 | 6.29 | 7.86 |
| 19:00 | 3532 | Ahi Nazareth vs Hapoel Acre | 2.27 | 3.03 | 3.33 |
| 19:00 | 3628 | Rosenborg BK 2 vs Kolstad | 2.40 | 5.09 | 2.06 |
| 19:00 | 3856 | Hapoel Rishon Lezion vs Ironi Tiberias | 1.88 | 3.40 | 3.95 |
| 19:00 | 3940 | Aalesund 2 vs Molde FK 2 | 1.73 | 4.32 | 3.44 |
| 19:30 | 4055 | Lorenskog vs Stromsgodset 2 | 2.16 | 3.74 | 2.70 |
| 20:00 | 1223 | Sonderjyske vs Vendsyssel FF | 1.63 | 3.77 | 4.50 |
| 20:00 | 1341 | FC Trollhattan vs Ljungskille | 2.25 | 3.15 | 2.95 |
| 20:00 | 1533 | Sarpsborg Sparta 2 vs Follo | 3.44 | 4.22 | 1.75 |
| 20:00 | 1798 | RW Essen vs Saarbrucken | 3.00 | 3.50 | 2.17 |
| 20:00 | 1909 | Stabaek Fotball 2 vs Grei | 1.31 | 5.48 | 6.46 |
| 20:00 | 2221 | CD Feirense vs Oliveirense | 1.82 | 3.44 | 4.09 |
| 20:00 | 2425 | Urozhay Krasnodar vs Arsenal Tula | 3.83 | 3.34 | 1.85 |
| 20:00 | 2660 | FK Haugesund 2 vs Djerv 1919 | 2.65 | 3.83 | 2.17 |
| 20:00 | 2947 | SC Kfar Qasem vs Maccabi Jaffa | 2.19 | 3.15 | 3.25 |
| 20:00 | 2951 | Sandnes Ulf 2 vs Viking FK 2 | 3.34 | 4.22 | 1.78 |
| 20:00 | 4101 | FC Rad vs Macva Sabac | 1.99 | 3.09 | 3.63 |
| 20:00 | 5307 | Umea IK W vs Pitea W | 4.04 | 3.45 | 1.78 |
| 20:00 | 5704 | Radnicki Nis vs Spartak Subotica | 1.85 | 3.38 | 3.78 |
| 20:00 | 5823 | Vittsjo W vs Linkopings W | 2.79 | 3.33 | 2.27 |
| 20:30 | 2336 | St Truiden U21 vs Westerlo U21 | 2.37 | 3.95 | 2.47 |
| 20:30 | 3206 | Oostende U21 vs AS Eupen U21 | 2.11 | 4.10 | 2.75 |
| 20:30 | 4758 | Argesul Pitesti vs CFR Cluj | 3.79 | 3.19 | 1.99 |
| 20:30 | 5679 | Waasland Beveren U21 vs Kmsk Deinze U21 | 1.62 | 4.60 | 4.10 |
| 21:00 | 1071 | RWD Molenbeek U21 vs Lommel U21 | 1.55 | 4.71 | 4.12 |
| 21:00 | 1687 | Deportivo Riestra vs Brown Adrogue | 1.88 | 3.01 | 4.24 |
| 21:15 | 5124 | Ready vs Kjelsaas 2 | 2.34 | 3.65 | 2.65 |
| 21:30 | 1135 | Alessandria vs AC Reggiana | 6.27 | 3.79 | 1.55 |
| 21:30 | 1828 | CA Fenix vs Los Andes | 2.51 | 2.85 | 2.85 |
| 21:30 | 5045 | Lujan vs Deportivo Laferrere | 2.55 | 2.75 | 3.10 |
| 21:30 | 5527 | Sportivo Barracas vs Deportivo Paraguayo | 1.75 | 3.38 | 4.32 |
| 22:00 | 3042 | Tenerife vs Malaga | 1.98 | 3.19 | 3.84 |
| 22:00 | 4286 | Concarneau vs FC Versailles 78 | 1.96 | 3.24 | 3.74 |
| 22:15 | 2447 | Stjarnan W vs Throttur Reykjavik W | 1.92 | 3.78 | 3.19 |
| 22:30 | 1913 | Arsenal Sarandi vs Aldosivi | 1.86 | 3.18 | 4.02 |
| 23:00 | 2845 | Real Santander vs Chico | 2.96 | 2.96 | 2.35 |
| 23:00 | 5355 | CA Boston River vs Danubio FC | 2.47 | 3.01 | 2.76 |
| 23:30 | 1061 | Ayacucho vs Alianza Atletico | 2.17 | 3.23 | 3.04 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatatu Septemba 19, 2022

Nipashe




Son afunguka mazito hat-trick

UKURASA 21

HAMNIWEZI...



Kiungo mshambuliaji wa Simba, Augustine Okrah, akiwatoka mabeki wa Nyasa Big Bullets ya Malawi kwenye mechi ya awali mkondo wa pili ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jana na wenyeji kushinda 2-0, hivyo kusonga mbele kwa jumla ya mabao 4-0 kutokana na mchezo wa kwanza kupata matokeo kama hayo ugenini. **PICHA: SIMBA**

## Mayele aahidi makundi CAF, Nabi awageukia

**Na Saada Akida**

LICHA ya kikosi chake kutinga kwa kishindo kwenye raundi ya kwanza ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi amesema ma hajaridhishwa na kiwango kilichooneshwa na safu yake ya ushambuliaji, lakini straika hatari wa timu hiyo, Fiston Mayele, akaahidi kuifikisha klabu hiyo hatua ya makundi.

Yanga juzi iliibuka na ushindi mnono wa mabao 5-0 dhidi ya Zalan FC ya Sudan Kusini, hivyo kuitoa timu hiyo kwa jumla ya mabao 9-0 kutokana na ushindi wao wa awali wa 4-0, huku Mayele akifunga hat-trick katika kila mchezo wa mechi hizo mbili.

Lakini Nabi amesema ana kazi kubwa katika hatua inayofuata kwa wachezaji wake kuwa makini kutumia nafasi wanazotengeneza kulingana na wapinzani watakaokutana nao katika hatua inayofuata ya michuano ya Ligi ya Mabingwa.

"Kama tungecheza na timu imara zaidi halafu tukafanya uzembe kama huu lazima ingetugharimu tumetengeneza nafasi nyingi za wazi hasa kipindi cha kwanza, lakini washambuliaji wangu wameshindwa kuzitumia hii ni mbaya na haijanifuraisha tunapaswa kubadilika.

Lakini Mayele alisema: "Nashukuru kwa kufunga hat-trick mbili, nashukuru Mungu na timu nzima, benchi la ufundi pia, tulipambana wote Mungu akanisaidia, tutaendela kupambana na mimi nitaendelea kupambania Yanga yetu ili isonge mbele. Najua imebaki mechi moja tuingie kwenye makundi kwa hiyo nawaomba Wanayanga waje kwa wingi, mwaka huu wachezaji tutapambana sana ili kuweza kupata kitu kizuri".

# Phiri aivusha Simba CAF

**Na Adam Fungamwango**

## Ni wakati Chama na Okrah wakifanya makubwa dhidi ya Big Bullets, sasa kuwavaa...

STRAIKA raia wa Zambia, Moses Phiri, aliyesajiliwa msimu huu kutoka Zanaco amefunga mabao mawili akiiwezesha Simba kutinga raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Nyasa Big Bullets, mechi ikichezwa jana Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**Phiri, ndiye aliyefunga bao la kwanza Septemba 10, mwaka huu kwenye Uwanja wa Bingu Mutharika, Lilongwe nchini Malawi, Simba ilipopata ushindi kama huo na kuifanya kusonga mbele kwa jumla ya mabao 4-0.**

Kwa ushindi huo, Simba sasa itacheza mechi ya raundi ya kwanza na mshindi kati ya Red Arrows ya Zambia na Primeiro de Agosto ya Angola.

Ni matokeo yaliyofanya Tanzania iwe na timu nne kwenye raundi ya kwanza, baada ya Yanga kuitoa Zalan FC kwa jumla ya mabao 9-0, Kipanga kuiondoa Al Hilal Wau ya Sudan Kusini kwa mikwaju 4-3 ya penalti, huku Azam yenyewe ikiwa imepita moja kwa moja kwenye raundi hiyo.

Dakika ya kwanza tu, tayari Simba ilikuwa imeshafika kwenye lango la Nyasa Big Bullets, Chama akijichanganya mwenyewe kutokana na pasi safi aliyopata kutoka kwa Augustine Okrah, kabla ya mabeki wa timu hiyo kuufagia mpira huo kwenye neo la hatari.

Kibu Denis aliingia na mpira kwenye eneo la hatari la wapinzani wao na kutoa pande kwa Phiri ambaye shuti lake liliwababatiza mabeki wa Nyassa Big Bullets na kutoka nje kuwa kona ambayo haikuzaa matunda.

Mohamed Hussein 'Tshabalala' angekuwa makini angeweza kuipatia Simba bao dakika ya 15 baada ya kuupokea mpira mrefu kwa kifua uliopigwa na Henock Inonga, kabla hajamzidi mbio John Lenjesi, lakini alipiga shuti ovyo ambalo lilitoka nje ya lango.

Kuona mashambulizi yanazidi, Nyasa Big Bullets ilifanya mabadiliko ya mapema kwa kumtoa Alick Lungu na kumuingiza Chimwemwe Idana.

Hata hivyo, bado haikuwa dawa kwani Simba iliendelea na mashambulizi mfululizo, Kibu akipaisha mpira karibu na lango baada ya krosi ya Okrah dakika ya 27, ndipo dakika moja baadaye bao lilipopatikana.

Mabeki waliokoa hatari kutoka kwa Adepoju Babatunde, na mpira mrefu ulipigwa kutoka langoni ulimkuta Clatous Chama ambaye alipiga pasi mpenyezo kwa Mzambia mwenzake iliyotangulia mbele na akawazidi mbio mabeki wa Nyasa Big Bullets kabla ya kuukwamisha mpira wavuni kulia kwa kipa Clever Mkungula.

Dakika tano baada ya mapumziko, Phiri alipachika bao la pili ambalo mazingira yake yakifanana na la kwanza.

Baada ya kuokoa shambulizi la Idana, ulipigwa mpira mrefu ambao Okrah alifanikiwa kuumiliki akiwa katikati ya mabeki, akamweka mfungaji ambaye naye alimrudishia, kabla ya kumpasia tena. Akiwa nje kidogo ya eneo la hatari, Phiri aliingia ndani kidogo na kuachia shuti la mguu wa kushoto lililokwenda moja kwa moja wavuni.

Kocha Juma Mgunda alifanya mabadiliko kwa kumtoa Inonga, Phiri, Kibu na Okrah, nafasi zao zikachukuliwa na Pape Sakho, Dejan Georgijevic, Nelson Okwa na Mohamed Ouattara.

Dakika za mwisho Nyasa Big Bullets ilionekana kuamka na kufanya mashambulizi na kupiga mashuti kadhaa kupitia kwa Ernest Peter na Antony Mfune, lakini Aishi Manula alikaa imara na kuokoa hatari hizo.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >